# Nipashe

Jumanne Aprili 18, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581284

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US





UKURASA 11


MID WEEK JACKPOT!

TZS. 553,549,430

KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SportPesa.CO.TZ

PIGA *150*87#





**Aliyekutwa** na nyeti tano za wanawake aachiwa huru mahakamani

UKURASA 3



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, ACP Alex Mkama akizungumza na waandishi wa habari mkoani humo jana, kuhusu hatua za kinidhamu zilizochukuliwa kwa askari wake watatu akiwemo Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani wilaya, ASP Aminiel Mosha kwa tuhuma za kumpiga dereva wa gari wakati wakiwa kazini maeneo ya Mikese. Picha ndogo: Maafande hao wakionekana kwenye gari dogo la dereva anayedaiwa kupigwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kigogo Trafiki aingia matatani

• **Yeye** na polisi wawili waponzwa na video ya kumpiga dereva... *Uk. 2*

## Mitandao yafungwa kwa kuhamasisha ushoga nchini

UKURASA 3



Rais Samia Suluhu Hassan akishuhudia Waziri wa Madini, Doto Biteko pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Jaji Eliezer Feleshi wakitiliana saini mkataba wa makubaliano ya msingi baina ya Serikali ya Tanzania na Kampuni ya Uchimbaji Madini ya Evolution Energy Minerals ya Australia iliyowakilishwa na Mtendaji Mkuu wake, Phillip Hoskins na Michael Bourgnoin, Ikulu Chamwino, mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

## Samia ataka umakini mikataba ya madini

UKURASA 2


**MICHEZO** ROBERTINHO ATOA SIRI YA KUIKANDA YANGA UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6



Mbunge Viti Maalumu, Halima Mdee akichangia hotuba ya mkadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Kigogo Trafiki matatani tuhuma za kumpiga dereva

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

JESHI la Polisi Mkoa wa Morogoro limechukua hatua za kinidhamu na kuwabadilishia majukumu askari wake watatu akiwamo Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Wilaya, ASP Aminiel Mosha kwa tuhuma za kumpiga dereva wa gari wakati akiwa kazini maeneo ya Mikese.

Tukio hilo lilirekodiwa na raia na kusambazwa kwenye mitandao ya kijamii.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Kamishna Msaidizi wa Polisi Alex Mkama alibainisha hayo jana alipojibu maswali ya waandishi wa habari waliofika ofisini kwake kutaka kufahamu iwapo aliona kipande hicho cha video kilichorekodiwa na kama aliwatambua askari waliofanya kitendo hicho na hatua zilizochukuliwa na Jeshi la Polisi.

"Hiyo clip (kipande cha viedo) ni kweli nimeona, na ni kweli hao ni askari wangu na tayari tumechukua hatua mbalimbali za kinidhamu ikiwamo kumbadilishia madaraka yake huyo askari aliyeonekana kumpiga dereva wakati hatua zaidi dhidi yake zikichukuliwa, na sio kwake yeye tu, na hao askari wengine walioonekana eneo la tukio ambao walikuwa wakiangalia tu," alisema.

Alitoa wito kwa dereva aliyefanyiwa tukio lile popote alipo alisaidie jeshi hilo kwa kufika kituo kikuu cha polisi, "aje aeleze kilichotokea na kama kuna madhara mengine aliyapata, yaweze kushughulikiwa kwa mujibu wa sheria".

Kamanda huyo alilaani tukio hilo kwa kuwa Jeshi la Polisi limekuwa likifanya kazi zake kwa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo mbalimbali na ndio maana wanaendelea na uchunguzi zaidi licha ya kuwabadilishia madaraka askari hao wakiongozwa na Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Wilaya.

"JESHI la Polisi linaongozwa na kusimamia na nidhamu, haki, uadilifu tunapoona mambo yanakwenda kinyume, ni lazima tuchukue hatua.

"Kama tulivyochukua kwa kumbadilisha majukumu wakati hatua zaidi za kinidhamu za ndani zikiendelea, PGO (Mwongozo wa Utendaji Kazi wa Polisi) inaelekeza vizuri kabisa, nani afanyiwe nini anapokosa, na sisi tumeshachukua hatua, hakuna maelekezo ya namna hii.

"Usiangalie lile tendo la mwisho tu na wale askari wengine lazima wachunguzwe, walikuwa na wajibu wa kufanya pale," alisisitiza Kamanda Mkama.

Tukio hilo lilianza kusambazwa mitandaoni Aprili 16 mwakahuu, majira ya asubuhi likionyesha askari polisi mwenye cheo cha nyota tatu (Mkaguzi wa Polisi) akimshambulia kwa kumpiga dereva wa gari dogo jeupe lenye namba za usajili T 117 DEU, huku baadhi ya watu wakisogea eneo hilo na haikujulikana mara moja sababu ya kipigo hicho.

Kitendo hicho kimelaaniwa na wadau mbalimbali wa usafirishaji, akiwamo Mwenyekiti wa Madereva Tanzania, Shubeti Mbakizao, aliyepaza sauti "ni vyema askari wachukuliwe hatua".

# Samia ataka umakini mikataba ya madini

**Na Christina Mwakangale**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema kuna haja kuwa makini na kuangalia aina ya washirika katika ushirikiano kwenye uendelezaji rasilimali za madini, ikizingatiwa Tanzania ni kati ya nchi zenye upekee wa madini adimu, kiasi cha kutupiwa macho na nchi kubwa duniani.

Akizungumza jana Ikulu mkoani Dodoma wakati wa utiaji saini makubaliano kati ya serikali na kampuni za uchimbaji wa madini adimu duniani yaliyopatikana nchini, Rais Samia alisema kuwa baada ya utafiti kubaini kuwapo kwa madini hayo, nchi inapaswa kuwa makini kunufaika nayo.

Kampuni ambazo zimeingia makubaliano na serikali jana, ni Evolution Energy Minerals Limited, EcoGraf Limited na Peak Rare Earth Limited, zote za Australia.

Rais Samia alisema utafiti wa madini aina ya kinywe na mengine yaliyo kwenye kundi adimu, ulianza mwaka 2000 kupitia kampuni mbalimbali na kwamba majibu yaliyopatikana, yanaonesha kuna tani milioni 67 zenye madini ya kinywe yaliyogundulika katika kijiji cha Chilalo mkoani Lindi yakitarajiwa kuchimbwa kwa miaka 18.

"Kama mnavyofahamu, nchi yetu imebarikiwa kuwa na madini mbalimbali kama graphite na ya kipekee kama kinywe, tunayo pia madini ya chuma, dhahabu, fedha, shaba, almasi, uranium na mengine mengi yaliyo nadra kupatikana.

"Madini haya hupatikana kwenye maeneo tofauti Lindi, Morogoro zipo katika ukanda wa madini ya kinywe na Mkoa wa Songwe upo katika ukanda adimu, na miradi hii ipo Kijiji cha Chilalo, pamoja na wilaya za Ulanga na Ngwala," alisema.

Alibainisha kuwa kumegundulika tani milioni 63 zenye wastani wa silimia 7.6 ya madini ya kinywe katika Kijiji cha Epanko, nayo yakitarajiwa kuchimbwa kwa muda kama huo.

Rais pia alisema tani milioni 18.5 zenye asilimia 4.8 za madini adimu zimegundulika katika Kijiji cha Ngwala mkoani Songwe, ambayo matarajio ni kuchimbwa kwa zaidi ya miaka 20.

"Madini haya ya kinywe na adimu yamo kwenye orodha ambayo yanajulikana na kama madini muhimu na ya kimkakati duniani. Yanahitajika sana katika teknolojia mpya ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, hutumika kutengenezea betri za magari ya umeme, vifaa vya kietroniki na mitambo mbalimbali.

"Tanzania tumejaliwa kuwa na madini hayo muhimu sana ya kimkakati kwa maenedeleo ya dunia, kwenye karne hii imeifanya nchi yetu kuangaliwa au kutamaniwa na wawekezaji wakubwa duniani," alisema.

Rais Samia alisema kwamba wakati wa ziara ya Makamu wa Rais wa Marekani, Kamala Harris, mazungumzo yao yaligusia suala la umuhimu wa madini hayo, ikiwamo mradi wa nikeli uliopo Kabanga pamoja na ujenzi kiwanda cha usafishaji madini kitakachojengwa Kahama mkoani Shinyanga.

"Madini haya yanakuza jina la Tanzania na hata nchi zenye nguvu duniani zinayaangalia. Siku zijazo nchi itakuwa kitovu cha usafishaji na usafirishaji wa madini haya... kijiografia tumezungukwa na nchi nane zenye madini kama ya kwetu.

Fursa zitatufikia, kutunufaisha kwa kuchakata madini na tuna njia za uhakika za kusafirisha madini haya.

"Fursa hizi tulizopewa na mwenyezi Mungu tusizichukulie kwa wepesi, bali itupe tumaini kubwa katika kuchagua nani wa kushirikiana naye katika kuvuna rasilimali hizo tulizobarikiwa na Mungu. Na tunazozawadiwa na mama yetu Tanzania kwa maslahi ya taifa letu.

"Mbali na umiliki wa hisa uliowekwa kisheria wa asilimia 16, serikali hunufaika kupitia kodi, tozo, ajira na maendeleo ya miundombinu na ukuaji wa kiteknolojia na urejeshaji hisani kwenye huduma za kijamii.

"Ninapongeza timu ya makubaliano ikiongozwa na Mwenyekiti wao Prof. Paramagamba Kabudi, pamoja na timu, sekretarieti na wizara, Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), Msajili wa Hazina," alipongeza Rais Samia.

Alisema ukuaji wa sekta ya madini nchini utaongeza ukuaji uchumi na kwenye Pato la Taifa (GDP), kupitia shughuli zilizopo kupitia sekta hiyo, ikiwamo sekta binafsi.

"Ninakumbuka mwaka juzi nilipomrudishia uwaziri wa madini, nilimwambia (Dotto Biteko) ifikapo 2020 sekta ya madini iwe inachangia asilimia 10 kabla ya 2025 sekta hii inakaribia kufikia asilimia 10, kwa jitihada hizi tutakapofika 2025 nina imani sekta itachangia zaidi," alisema Rais.

Mkuu wa Nchi pia alisema wachimbaji wadogo wamejumuishwa na sasa mchango wao kwenye sekta hiyo unaonekana, akiwataka waachane na utoroshaji wa madini kwa kuwa viwanda vya uchakataji vipo.

"Kinamama wenzangu na kinababa tunaopenda kupika, mwende kulisha na kwenda kwenye migodi hii... na LNG inakuja, wajipange kwenda kutoa huduma. Tuna mtindo ndugu zangu wawekezaji mnachukua miradi, mnakwenda kuweka fedha 'stock exchange' na kutengeneza fedha kwanza, ndipo turudi kuwekeza... huu ni uhujumu uchumi, ninataraji hili halitotokea," alionya.

Waziri wa Madini, Dotto Biteko alisema makubaliano hayo yataleta mchango wa mtaji nchini kwa dola za kimarekani milioni 667, akiitaja ni miradi mikubwa iliyo kwenye mkakati inayohitajikia duniani.

"Hujawaacha wachimbaji wadogo, Mheshimiwa Rais wachimbaji hawa walikuwa wanachangia asilimia 20 ya mauzo yote wakati ulipoingia madarakani, lakini katika 'study' ya mwisho tumeona uchangiaji wao sasa ni kwa asilimia 40," alisema waziri huyo.

## HABARI KITAIFA



Waziri wa Maji, Jumaa Aweso (katikati), akijadiliana jambo na Mkuu wa Wilaya ya Korogwe, Jokate Mwegelo alipofanya ziara wilayani humo, mkoani Tanga juzi, kwa ajili ya kuangalia tatizo la upatikanaji wa maji. **PICHA: OSCAR ASSENGA**

# Serikali yaifunga mitandao ya kijamii kwa kuhamasisha ushoga

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye amebainisha idadi ya mitandao ya kijamii iliyofungiwa kutokana na kuhamasisha mapenzi ya jinsia moja kupitia akaunti zao.

Mitandao hiyo iliyofungiwa ni pamoja na tovuti 334, akaunti za Facebook 361, akaunti za Twitter 12, vikoa zaidi ya 2,456 na Instagramu 198.

Nape alibainisha hayo jana bungeni jijini hapa alipoongezea majibu ya swali la Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Anatropia Theonest.

Mbunge huyo alitaka kujua hatua zinazochukuliwa na serikali dhidi ya watu wanaohamasisha mapenzi ya jinsia moja na kama ipo tayari kuleta bungeni muswada wa marekebisho ya Sheria ya Makosa ya Jinai na Makosa ya Kujamiiana ili kama kuna upungufu urekebishwe.

Waziri Nape aliliambia Bunge kuwa hakuna matangazo ya mapenzi ya jinsia moja kwenye vyombo vya habari ambayo yanaruhusiwa na serikali ipo makini katika hilo.

Alisema kulikuwa na tatizo la vyombo vya habari vya mitandaoni na tayari hatua za kuvifungia imeshafanyika na kuitaka jamii kuchukua hatua kuanzia kwenye ngazi ya familia.

Awali akijibu maswali hayo ya nyongeza, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Pauline Gekul alisema sheria zilizopo zinafanya kazi kuhakikisha wanaobainika wanachukuliwa hatua, akisisitiza "wapo waliofungwa".

Alisema serikali iko tayari kufanya marekebisho endapo yatahitajika baada ya utafiti kufanyika kwenye sheria zilizopo kama alivyoelekeza Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson wiki iliyopita.

Katika swali la msingi, mbunge huyo alitaka kujua sheria za Tanzania zinasema nini kuhusu uhusiano wa jinsia moja.

Gekul, akijibu swali hilo, alisema sheria za Tanzania haziruhusu uhusiano wa jinsia moja na kwa mujibu wa kifungu cha tisa cha Sheria ya Ndoa kinachotafsiri ndoa ni uhusiano wa hiyari kati ya mwanamume na mwanamke.

Alisema kifungu cha 154 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura ya 16 kinabainisha kuwa kufanya mapenzi kinyume cha maumbile ya jinsia ni kosa la jinai ambalo adhabu yake ni kifungo cha maisha jela au kifungo kisichopungua miaka 30 jela.

# Aliyekutwa na nyeti tano za wanawake aachiwa huru

**Na Grace Gurisha**

MKAZI wa Maswa mkoani Simiyu, Salum Nkonja, aliyekuwa anatuhumiwa kukutwa na sehemu za siri tano za kike na chuchu mbili za wanawake, ameachiwa huru mahakamani baada ya kesi hiyo kuahirishwa mara kwa mara.

Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam imeamuru vielelezo hivyo ambavyo ni mafuvu mawili ya binadamu, sehemu za siri tano za kike na chuchu mbili ziharibiwe kwa sababu tayari zilikuwa zimekauka.

Uamuzi huo ulitolewa jana na Hakimu Mkazi Mkuu Ramadhani Rugemalira wa mahakama hiyo wakati kesi hiyo ilipoitwa kwa ajili ya kusikilizwa kwa shahidi wa upande wa mashtaka, lakini ilishindikana kwa sababu ya vielelezo havikuwapo.

Hakimu Rugemalira alisema kwa mara ya kwanza mshtakiwa huyo alifikishwa mahakamani mwaka 2017 na alifunguliwa kesi ya mauji namba 21 ya mwaka huo.

Alidai kuwa kesi hiyo iliendelea hadi Novemba 19, 2020, Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP) alipowasilisha mahakamani hati ya kutokuwa na nia ya kuendelea na mashtaka dhidi ya mshtakiwa.

"Lakini tarehe hiyo alikamatwa tena na kufunguliwa tena kesi ya uhujumu uchumi namba 88 ya mwaka 2020 ambayo iliendelea hadi Juni 7, 2022 ambapo mshtakiwa aliachiwa na mahakama chini ya kifungu namba 225.

"Baada ya kuachiwa, alikamatwa tena ambapo alikaa zaidi ya siku 14 mahabusu na Juni 21, 2022 alirudishwa tena mbele ya mahakama hii na kufunguliwa kesi nyingine ya uhujumu uchumi namba 32 ya mwaka 2022," alisema.

Hakimu huyo alisema kesi hiyo tangu mwezi Juni mwaka jana imekuwa ikiahirishwa mara kwa mara kwa kutokufika kwa mashahidi wa upande wa mashtaka, pia shahidi anaweza kufika lakini vielelezo hakuna, hivyo kesi kuahirishwa.

Hakimu Rugemalira alisema kesi hiyo ilipitia maahirisho ya mwisho zaidi ya mara tano na jana shahidi alikuwapo lakini hakuweza kuendelea na ushahidi kwa kuwa vielelezo havikuwasilishwa.

"Shahidi huyu wa leo (jana) Koplo Seleman alifika mahakamani Oktoba 19, 2022 na Desemba 8,2022 hakutoa ushahidi wake kwa sababu vielelezo havikuwapo.

"Hali hii haiwezi kuvumiliwa na mahakama ukizingatia mshtakiwa naye ana haki zake, katika waraka wa DPP unaeleza kuwa katika mashauri ya jinai kesi ikifika mahakamani, upelelezi uwe umekamilika," alisema.

Pia alisema katika mabadiliko ya sheria za jinai yameelekeza kwamba mashauri yanayoondolewa na yasirudishwe mahakamani kama upelelezi wake haujakamilika.

"Kwa mujibu wa sheria, hatuwezi kuulazimisha upande wa mashtaka kufunga ushahidi wake, lakini mahakama ina mamlaka kuwa ikiona sababu zinazotolewa za kuahirisha kesi sio za msingi inafuta shtaka hilo ili haki itendeke.

"Kutokana na mazingira haya, mshtakiwa alishakaa gerezani zaidi ya miaka mitano akiwa mahabusu, kwa mamlaka ninaifuta kesi hii sio kwa kifungu namba 225, yaani mshtakiwa asikamatwe tena labda hadi pale watakapopata ushahidi na vielelezo na pia rufani iko wazi kwa ambaye hajaridhika," alisema Hakimu Rugemalira.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Grace Mwanga alidai kuwa ana shahidi mmoja, lakini wanaomba tarehe nyingine ya kusikilizwa kwa sababu vielelezo hakuna, ambapo Wakili wa Mshtakiwa, Mohamed Majaliwa alipinga suala hilo.

Ilidaiwa kuwa Oktoba 30, 2017, Wilaya ya Ubungo, Dar es Salaam, mshtakiwa huyo alikutwa na sikio na pembe ya nyati, vyote vikiwa na thamani ya Sh. 4,318,700 bila kibali kutoka kwa Mkurugenzi wa Wanyamapori.

Alidai kuwa katika tarehe na eneo hilo, mshtakiwa huyo pia alikutwa na uume wa mbwamwitu wenye thamani ya Sh. 2,272,600 pamoja na uume wa nyumbu wenye thamani ya Sh. 1,477,450 bila kibali.

Ilidaiwa kuwa Novemba 30, 2017, Wilaya ya Ubungo, Dar es Salaam, mshtakiwa huyo alikutwa na mikia mitano ya ngiri yenye thamani ya Sh. 5,114,250, uume wa fisi watatu wenye thamani ya Sh. 3,750,450.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
18.04.2023

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya Jumatano tarehe 19-04-2023 kampuni ya Mainline Carriers Ltd itasafirisha Mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka Dar-Es-Salaam Port kuelekea Rufiji, gari hiyo ina namba za usajili: **T 975 DTN / T 777 AQR**
2. Gari hiyo ina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - mita 19.00**
   **Upana - mita 5.10**
   **Kimo - mita 4.60**
3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam, Pwani hadi Rufiji kupitia Kibiti,** gari itasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

217380802

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***



Victoria FINANCE

Victoria Finance Plc
5th Floor, Sky Tower Building-Kijitonyama
New Bagamoyo Road
P.O.Box 12102, Dar es Salaam - Tanzania
Telephone +255 22 277 4577
Fax: +255 22 277 4559
Email: info@victoriafinance.co.tz
Website: www.victoriafinance.co.tz

**TANGAZO LA MINADA YA HADHARA**

VICTORIA FINANCE PLC INAPENDA KUUTANGAZIA UMMA YA KWAMBA KWA IDHINI ITAKAYOTOA KWA KAMPUNI TOFAUTI ZA UDALALI INATARAJIA KUUZA KWA MNADA WA HADHARA DHAMANA ZA WADAIWA SUGU KAMA IFUATAVYO;

| NA | JINA LA MDAIWA | DHAMANA | AINA NA SEHEMU YA DHAMANA | DALALI | TAREHE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | CRISPIN FRANCIS OCHANDA | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO - GOBA | J & J RECOVERIES | 02-05-2023 |
| 2 | HASSAN JUMA MRISHO | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO - DAKAWA | HOLLYNESS & RESPISHERS LTD | 02-05-2023 |
| 3 | SADA ABDALLAH LAISER | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO - TEGETA | J & J RECOVERIES | 02-05-2023 |
| 4 | TIMOTHEO SAYI LIMBU | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO - TABATA | AMA'Z AUCTION MART | 02-05-2023 |
| 5 | JACQULINE TESHA AS AN ADMISTRATOR OF THE ESTATES OF THE LATE CHIEDRICK KOMBA JARIBUNI | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO - TABATA KINYEREZI | J & J RECOVERIES | 02-05-2023 |
| 6 | JACQULINE TESHA AS AN ADMISTRATOR OF THE ESTATES OF THE LATE CHIEDRICK KOMBA JARIBUNI | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO- TABATA KINYEREZI | J & J RECOVERIES | 02-05-2023 |
| 7 | PATRICK KENDAMVANO JULIUS | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO - KIBAMBA | J & J RECOVERIES | 02-05-2023 |
| 8 | MODESTUS IBRAHIMU MELEO | NYUMBA | LESENI YA MAKAZI - MBAGALA | LEGENDS AUCTION MART | 02-05-2023 |
| 9 | PENDO SISTY CHUWA | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO - MBEZI BEACH JOGOO | LEGENDS AUCTION MART | 02-05-2023 |
| 10 | AMANI MUSSA MTULI | NYUMBA | LESENI YA MAKAZI - NZASA KILUNGULE | DIAMOND CREDIT RECOVERY CO LTD. | 02-05-2023 |
| 11 | NASHON MARWA NYAMUHANGA | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO - BUZA MAKANGARAWE | DIAMOND CREDIT RECOVERY CO LTD. | 02-05-2023 |
| 12 | SAID JUMA TAMAMBELE | NYUMBA | LESENI YA MAKAZI - MAKURUMLA KAGERA | J & J RECOVERIES | 02-05-2023 |
| 13 | CHARLES ODEN MWAIOLA | NYUMBA | OFA YAHATI MILIKI - KIBAHA | LEGENDS AUCTION MART | 02-05-2023 |

Minada yote itafanyika mahali husika katika muda na siku ambayo itatangazwa kupitia katika vipeperushi na magari ya matangazo kutokana na idhini itayotoka kutoka katika vyombo husika vya Serikali.

**MASHARTI YA MNADA;**
- Asilimia 25% ya bei iliyofikia italipwa papo hapo na asilimia 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne. (14). Kwa kushindwa kufanya hivyo itapelekea mnada kurudiwa tena na pesa zilizolipwa kutokurudishwa.
- Gharama za kumuhamisha mmiliki na kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.
- Dhamana itauzwa Kama ilivyo.

# Mawakala CRDB kuanza kutoa huduma za bima

**Na Mwandishi Wetu**

IKITIMIZA miaka 10 tangu uanzishwaji wa mfumo wa utoaji huduma wa CRDB Wakala, Benki ya CRDB imetangaza kuanzisha huduma za bima kupitia mawakala wake ikiwa ni mkakati wa kusaidia jitihada za serikali kukuza ujumuishi wa bima nchini.

Naibu Kamishna wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima nchini (TIRA), Khadija Said, amepongeza mkakati huo, akisema utasaidia kufanikisha lengo la serikali la kuongeza ujumuishi wa bima kutoka asilimia 15 hivi sasa kufikia asilimia 50 ifikapo mwaka 2030.

"Ninatambua kuwa Benki ya CRDB ndio kinara kwa idadi ya mawakala katika sekta ya benki ikiwa na CRDB Wakala zaidi ya 25,000 nchi nzima. Kwa idadi hii, ni dhahiri kuwa kasi ya ufikishaji na ufikiaji wa huduma za bima itakwenda kuongezeka kwa kiasi kikubwa," alisema Naibu Kamishna wa TIRA huku akiwataka mawakala kufuata miongozo iliyowekwa.

Naibu Kamishna pia aliipongeza Benki ya CRDB kwa mapinduzi makubwa ambayo imeyafanya katika sekta ya fedha nchini katika kipindi cha miaka 10 ya CRDB Wakala. Alisema CRDB Wakala imetoa mchango mkubwa katika kufikisha huduma za fedha kwa wananchi.

Alipongeza benki hiyo kwa kuboresha huduma zinazopatikana kupitia CRDB Wakala ambapo sasa hivi wateja wanaweza kupata zaidi ya asilimia 95 ya huduma kupitia mfumo huo ikiwamo huduma ya kufungua akaunti zote za benki, ikiwamo akaunti za Al Barakah, zinazofuata misingi ya sheria.

"Niwapongeze pia kwa uzinduzi wa kampeni ya '10 na Kitu' ambayo inakwenda kutoa elimu kwa wananchi juu ya huduma zinazotolewa kupitia CRDB Wakala ikiwamo huduma za bima. Niwaombe mawakala tukashiriki kikamilifu," alisema.

Akiizungumzia kampeni ya '10 na Kitu', Mkurugenzi wa Wateja Wadogo na wa Kati wa Benki ya CRDB, Bonaventura Paul alisema mbali na kusherehekea maiaka 10 ya CRDB Wakala, kampeni hiyo pia inalenga kuhamasisha mawakala kuongeza kasi ya utoaji huduma kwa kufanya miamala mingi zaidi ili kuchochea ujumuishi wa kifedha.

"Kila mwezi tutakuwa tukitoa zawadi kwa CRDB Wakala ambao watakuwa wamefanya miamala mingi, kufungua akaunti nyingi, na kuuza huduma za bima. Jumla ya zawadi zote katika kampeni hii ni pikipiki 40, bajaj tano na gari aina ya Toyota Alphad kwa mshindi wa jumla," alibainisha.



Baadhi ya wafanyabiashara wa Soko la kwa Bintikaenga, mtaa wa Matokeo, kata ya Mabibo, Dar es Salaam, wakiokota mabaki ya vitu vyao baada ya nyumba na mabanda yao ya biashara kuvunjwa sokoni hapo jana, kwa amri ya mahakama. **PICHA: JENIFER GILLA.**

## Wafanyabiashara wataharuki kukuta soko lao limevunjwa

**Na Jenifer Gilla**

WAFANYABIASHARA katika Soko la Binti Kaenga, lililopo katika Mtaa wa Matokeo, Kata ya Mabibo, jijini Dar es Salaam, wamelalamikia kuvunjiwa vibanda vyao saa 10 alfajiri jana bila kupewa taarifa za kuondoa mali zao hali iliyowasababishia hasara, kutokana na mgogoro kati ya wamiliki wa eneo hilo na ofisi za Chama cha Mapinduzi (CCM) ya kata hiyo.

Mfanyabiashara wa nafaka, Esther Banigwa, alisema amepata hasara Sh. milioni nne kutokana na adha hiyo, kwa kuwa hakupata muda wa kujiandaa na kutoa mali zilizokuwapo kwenye kibanda. Alisema alikuja kugundua kuvunjwa kwa eneo hilo saa moja alfajiri jana alipokuwa anakwenda katika eneo hilo kwa ajili ya kuendelea na biashara yake ya kila siku inayomsaidia kuhudumia familia yake na kulipa marejesho ya mikopo aliyochukua kwa ajili ya kutanua biashara hiyo.

"Sikupata taarifa yoyote kwa kuwa tangu jana simu yangu ilikuwa imezima kutokana na kutokuwa na chaji, baada ya kufika hapa nikiwa na mizigo yangu ya kuongezea kwenye biashara nakuta watu wamekusanyika wanaokota mabaki, kwa kweli nilipatwa na mshtuko. Kulikuwa na shida gani kama tungetaarifiwa tukaondoa vitu vyetu?" Alihoji Esther kwa uchungu.

Mfanyabiashara wa mashine ya kusaga nafaka, Bensel Kisako, alisema amepata hasara kubwa ikiwamo kuharibika kwa mashine za kusaga nafaka, nafaka kuingia mchanga na kutofaa tena kwa biashara jambo lililomrudisha nyuma kiuchumi na kimaendeleo.

Naye mfanyabiashara wa Molel Batholomayo, alisema kitendo kilichofanyika na hakikuwa cha busara kwa kuwa kimewatia hasara ambayo ingeweza kuzuilika ukizingatia kuwa wao ni wapangaji na wamelipa kodi kufanya biashara katika eneo hilo.

"Huu mgogoro tunaufahamu ni wa muda mrefu, lakini kama kulikuwa na amri ya mahakama ya kuvunjwa ilipaswa wapangaji tupewe taarifa ili tuondoe vitu vyetu tusipate hasara, hiki kilichofanywa hapa ni uonevu mkubwa na ukiukwaji wa haki za binadamu, sidhani kama nitaiangalia CCM kwa jicho la zamani," alisema.

Mwenyekiti wa serikali ya mtaa huo, Mfaume Mtikaliyoni alisema alipigiwa simu na kampuni ya udalali kuwa wamepewa kibali na Mahakama cha kuvunja eneo hilo na kwa cheo chake hakuwa na mamlaka ya kuzuia amri hiyo.

Mfaume, ambaye pia ni Mjumbe wa Siasa wa CCM Tawi la Matokeo, alisema kwa taarifa alizonazo ni kuwa kesi ilishaisha tangu kwaka 2019 na hakuna rufaa yoyote iliyokatwa lakini aliwapa taarifa ya kuwataka waondoke eneo hilo mara mbili na hawakutii.

"Nilifanya jitihada kama mwanachama (wa CCM) na kama kiongozi wa mtaa kuhakikisha kuwa inapatikana notisi ya mahakama ya kuwataarifu waondoke katika eneo hilo, na ikapatikana nikawakabidhi wamiliki wa eneo hilo mkononi, wapo waliokataa kupokea, nikaongea na mwanasheria akaniambia nibandike ukutani, nikabandika wakaichana na wengine wakanitukana," alisema.

Alisema alijaribu kuwahoji waliopewa kazi ya kuvunja eneo hilo kama wametoa taarifa kwa wahusika wakamjibu kuwa hawakufanya hivyo kwa kuhofia usalama wao kwa kuwa baadhi ya watu wakipewa taarifa hukimbilia kuwadhuru kwa nia ya kuwazuia.

## Mkwawa yatoa mil. 20/- kwa yatima, Magereza

**Na Mwandishi Wetu,** TABORA

KAMPUNI ya Mkwawa Leaf Tobacco Limited, imekabidhi vifaa vya zaidi ya Sh. milioni 20, kwa vituo viwili vya watoto na Magereza mbili mkoani hapa.

Pia, kampuni hiyo imefuturisha waislam wakiongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Dk. Batilda Buriani.

Dk. Buriani aliipongeza kampuni hiyo kuwajali wengine kwa kuwapa misaada mbalimbali na chakula.

"Ninaahidi kushirikiana na kampuni hii ya Mkwawa katika kuendeleza zao letu la tumbaku ambalo hapo awali liliporomoka sana, tutasimamia kila kipengele katika mnyororo wa thamani ikiwamo utunzaji wa mazingira na kuhakikisha kuwa ukaushaji wa zao unatumia miti ya kupanda na sio miti pori," alisema.

Kuhusu mmomonyoko wa maadili katika jamii, aliwaasa wazazi kuongeza muda wa kukaa na watoto wao na kuboresha malezi, akiahidi kuwasaka wote wanaowarubuni vijana kujiingiza katika matendo mabaya ikiwamo ushoga na usagaji.

Mkurugenzi Mkuu wa kamapuni hiyo, Matthew Kapnias, alisema wametoa kwa watu wenye uhitaji ili kuwasaidia katika kipindi hiki cha kuelekea mwisho wa mwezi mtukufu wa Ramadhani.

Alisema wameona ni vyema aanze kazi kwa kutoa msaada kwa wahitaji kama sehemu ya ibada yake kwa Mungu na kuomba baraka zake.

Pia, kampuni yake imekusudia kushirikiana kwa karibu na serikali upandaji miti ili kilimo hicho kisiharibu mazingira na kupambana na utumikishaji watoto katika mashamba ya tumbaku ili zao hilo lisiwe la lawama.

Shekhe Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Ibrahim Mavumbi, alisema sadaka njema kwa Mwenyezi Mungu ni kuwapatia furaha watu wasiojiweza na maskini, jambo ambalo kampuni hiyo wamelifanya.

Mkurugenzi Msaidizi wa Kampuni hiyo, Richard Sinamtwa alivitaja vitu vilivyotolewa kuwa mchele kilo 3,000, sukari mifuko 50, mafuta ya kula ndoo 20, sabuni katoni 50, karanga kilo 125 na nyembe dazani 400, magodoro 115, mashuka 280 na neti 185.

"Bidhaa zote hizi zimegawanywa kwenye vituo hivyo vinne yaani magereza mbili na vituo vya watoto vya kulelea viwili, kimoja cha kikristo na kingine cha kiislamu," alisema.

Kaimu Mkuu wa Gereza Kuu wa Uyui, Mrakibu Mwandamizi wa Jeshi la Magereza, Richard Malifedha na Mkuu wa Gereza la Mahabusu Mrakibu Mwandamizi wa Jeshi la Magereza, Ally Lipululu walishukuru kwa sadaka hiyo ya wafungwa na kuomba waendeleea kutoa zaidi kwa wahitaji.

Akipokea msaada kwa niaba ya kituo chake cha mama Thereza, Sista Jenny Charenty alisema wanaishukuru kampuni hiyo kwa kutoa misaada hiyo na kwamba umekuja kipindi ambacho walikuwa wana uhitaji mkubwa wa neti pamoja na chakula.

Msimamizi wa kituo Igambilo Islamic Opharnage Centre, Abdulhamiid Willah, alishukuru kampuni hiyo ambayo alisema imetafasiri maneno ya Mtume kwa vitendo cha kuwajali na kuwathamini watoto yatima na wajane.

HABARI KITAIFA

# Wagonjwa wa moyo 350 wapokewa JKCI kila siku

**Na Christina Mwakangale**

DAKTARI Bingwa wa Moyo wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Pedro Pallangyo, amesema idadi ya wagonjwa wanaofika kwa siku katika taasisi hiyo kwa ajili ya kupata matibabu ni wastani wa 300 hadi 350.

Amesema wengi wao chanzo kikuu ni mtindo wa maisha ikiwamo matumizi ya vilevi, sigara na mlo wa mafuta uliokithiri.

Alibainisha hayo katika ufafanuzi wake kuhusu utendaji wao wa kazi, akieleza kuwa mafuta yanapoingia mwilini huganda kwenye mishipa ambayo inasambaza damu mwilini na kwenye moyo.

Dk. Pallangyo alisema: "Picha ambayo tunaiona zaidi kwenye tafiti za moyo, ni mishipa ya moyo kuziba, ina hatua mbalimbali. Hatua za awali inaweza kuwa asilimia 10 hadi 20 na katika hatua hiyo mtu anaweza kutohisi dalili zozote.

Aliongeza: "Kuanzia asilimia 30 hadi 40 mtu anaweza kujisikia hali ya kuchoka ambayo haielezeki, ikizidi hapo anashindwa hata kufanya shughuli zake za kawaida, ikifika asilimia 70 na kuendelea mhusika anaweza kupata vichomi au maumivu kwenye moyo".

Anafafanua kwamba mtu anapofikisha asilimia 100 anaweza kukubwa na kifo cha ghafla.

Alisema waliowafanyia uchunguzi kwenye taasis hiyo, mmoja kati ya wawili hukutwa na tatizo la mishipa ya damu kuziba na kuhitaji kuzibuliwa ili kurejea kwenye hali zao za awali.

"Bahati mbaya mtambo unaotumika kufanya vipimo vya moyo hapa nchini unapatikana Mkoa wa Dar es Salaam na Dodoma, hivyo wanaotoka mbali na maeneo hayo wakipata tatizo la mishipa kuziba kwa asilimia 100 inakuwa ngumu kuokoa maisha yao kwasababu ya umbali wa kufika katika mikoa hiyo kupata matibabu ya haraka," alisema.

Dk. Pallangyo ambaye pia ni Mkuu wa Kitengo cha Utafiti na Mafunzo JKCI, alisema hakuna dalili maalum za awali kwa mtu mwenye tatizo la moyo na kwamba zilizopo zinafanana na zilizopo katika magonjwa mengine.

"Unaweza kusema ni kichomi au maumivu ya kwenye moyo, ambayo nayo yakijitokeza inamaanisha tatizo limeanza kuwa kubwa na inawezekana mishipa imeshaziba kwa zaidi ya asilimia 50," alisema na kuongeza:

"Mafuta ya aina yoyote kiwango kikizidi kwenye damu italeta hiyo shida bila kujali ni ya aina gani, lakini yanayoweza kuwa na athari zaidi ni yanayotokana na wanyama, ndiyo maana inashauriwa kutumia mafuta ya mimea kama alizeti japokuwa haimaanishi yenyewe ni salama zaidi kwa sababu yakizidi tatizo linakuwa ni lilelile".

Alisema kinachotakiwa kufanyika ni kupunguza aina ya vyakula ambavyo vinakuwa na mafuta mengi kwa kuwa mazingira ya hivi sasa yamekuwa yakiwalazimisha watu kula vyakula vya aina hiyo.

Alisema: "Mfano unapokuwa nyumbani na unaandaa chakula mwenyewe, unaweza kuacha kutumia mafuta katika vyakula ambavyo si lazima utumie mafuta. Kwa wanaopenda kula vyakula vya kulowekwa kwenye mafuta kama chips na vinginevyo wajitahidi kupunguza idadi ya siku ambazo wanakula milo ya aina hiyo.

"Ni kweli lakini tatizo ni kuwa kiwango cha mazoezi kinachofanywa na wengi kuondoa mafuta mwilini ni kidogo kuliko uhalisia wa mafuta wanayoingiza, ni wachache wanaoweza kutimiza kiwango cha mazoezi ya kutoa mafuta, ikawa zaidi ya kiwango cha mafuta wanachoingiza," alisema Dk. Pedro.

Alisema unywaji pombe hutanua moyo na kuwa mkubwa kisha kushindwa kufanya kazi ipasavyo kutokana na damu kuwa na kiwango kikubwa cha kilevi ambacho ni sumu.

Mtaalamu huyo alisema aina zote za vilevi zina madhara bila kujali ni za viwandani au za kienyeji.

Alisema: "Mwanaume anashauriwa kutozidisha kunywa chupa tatu, mwanamke anashauriwa kutozidisha chupa mbili. Unywaji wa wine hapo siyo suala la chupa bali glasi, inashauriwa kutozidisha glasi moja na pombe kali haitakiwi kuzidisha shoti moja".

# Gambo aibua tuhuma nzito ubadhirifu mabilioni Arusha

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

MBUNGE wa Arusha Mjini (CCM), Mrisho Gambo, ameibua tena tuhuma nzito za ubadhirifu wa mabilioni ya fedha za umma kwenye mradi wa ujenzi wa jengo la utawala la ghorofa zaidi ya sita katika Halmashauri ya Jiji la Arusha.

Kutokana na tuhuma hizo, amemwomba Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angellah Kairuki na timu yake, kuokoa fedha hizo.

Akichangia jana bungeni jijini hapa mjadala wa bajeti ya makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/24, Gambo alisema katika Halmashauri ya Jiji la Arusha, kuna changamoto kubwa ya ubadhirifu wa fedha za halmashauri.

"Kwenye Jiji letu la Arusha, tuna changamoto kubwa sana ya ubadhirifu wa fedha za halmashauri. Nitapenda nitoe mifano michache kabla sijaenda kwenye uhalisia. La kwanza, tunajenga jengo la utawala la ghorofa zaidi ya sita, lakini bado wametafuta fundi mjenzi bila kutangaza tenda (zabuni).

"Taratibu za manunuzi hazijafuatwa; wamemtafuta tu rafiki yao wamemuweka pale amesaini mkataba wakampa kazi ya Sh. 199,750,000, lakini pia bado wamenunua vifaa vya Sh. milioni 132, ambavyo havijathibitika kufika eneo la site.

"Ukiangalia pia, bado wameenda kuongeza nondo za ziada ya tani 6.48 zenye thamani ya Sh. milioni



17, ambazo zinatokana na uzembe wa wataalamu wetu. Wameongeza malipo ya Sh. milioni 21 kwa fundi kutokana na uzembe pia wa wataalamu wetu. Wameanza ujenzi huo bila kuwa na mtaalamu mshauri katika ujenzi huo ambao nazungumzia wa jengo la utawala."

Mbunge huyo, alisema katika jiji hilo kumekuwa na malipo feki, ikiwamo risiti feki za EFD (stakabadhi ya mashine za kielektroniki) za Sh. 699,945,471.

"Hela zimetoka, wamefoji risiti wamepeleka halmashauri na tumekosa kupata huduma. Lakini bado pia wameenda kutengeneza quotation za kughushi za shilingi 580,545, 900 (anaitaja kampuni), ambayo ni Sh. milioni 543 na (anaitaja kampuni nyingine) Sh. milioni 36.

"Lakini bado pia, wamefanya malipo ya Sh. 36,580,000 kwa wazabuni ambao hawakutoa huduma yoyote katika Jiji la Arusha, na mbunge akizungumza wanasema huyu mbunge anagombana na watu. Kwenye mambo kama haya, lazima tugombane. Lakini pia kumekuwa na manunuzi ya shilingi 12, 822,400 kupitia dokezo ambalo wanasema liliandikwa na mtu anaitwa (anamtaja), lakini baada ya kuitwa, amekana dokezo hilo. Kwa hiyo hilo dokezo limeonekana ni feki, lakini mchakato uliendelea.

"Pia, bado kumekuwa na matumizi ya fedha za masurufu, Sh. milioni 62, ambayo pia yanaviashiria vya ubadhirifu na kulikuwa pia na matumizi ya Sh. milioni 132, ambazo gharama zake hazina sapoti yoyote ya matumizi. Wanachukua hela wanatumia, hawajali, kwa sababu wanajua ngazi ya mkoa na ngazi ya wilaya, wala hawana cha kuwafanya, na pengine inaweza ikawa ni sehemu ya changamoto hizo."

Vilevile, alisema katika Jiji la Arusha kumekuwa na matumizi ya ununuzi wa bidhaa mbalimbali, Shilingi bilioni mbili ambayo hayana uthibitisho na wala matumizi yake hayaelezeki.

"Mheshimiwa Mwenyekiti, haya masuala ni makubwa sana; nadhani ni vizuri waziri wa TAMISEMI, na timu yake wakafanye utaratibu wa kwenda kuweka jicho la ziada kwenye jiji letu ili tuweze kuokoa hizi fedha za umma.

"Kumekuwa na matumizi pia ya akaunti ya amana yaliyokosa uthibitisho ya Sh. 92,692, 714.

"Nimesema nianze na utangulizi huo kwa sababu Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Jiji letu limekuwa ni shamba la bibi. Watu wameungana...kuimaliza Halmashauri yetu. Mimi nimejitoa kafara kuhangaika na masuala haya ili kulinda maslahi mapana ya wananchi wetu."

# Kesi ya kina Mdee Mjumbe Bodi ya Wadhamini CHADEMA kuhojiwa leo

**Na Grace Gurisha**

JOPO la mawakili wanaowatetea wabunge 19 wa Viti Maalum kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) katika kesi ya kupinga kuvuliwa uanachama, leo linatarajia kumuuliza maswali ya dodoso mjumbe wa Bodi ya Wadhamini wa chama hicho, Lucy Mollel.

Jopo hilo linajumuisha mawakili Ipilinga Panya, Aliko Mwamanenge, Edson Kilatu, Emmanuel Ukashu, Joyce Mwakakila na Afrey Maunga, ambao watamuhoji mjumbe huyo mbele ya Jaji Cyprian Mkeha wa Mahakama Kuu, Masjala Kuu Dar es Salaam.

Mollel ataulizwa maswali kutokana na kiapo kinzani alichokiwasilisha mahakamani hapo katika kesi iliyofunguliwa na Mbunge wa Viti Maalum, Halima Mdee na wenzake 18 wakiomba mahakama ipitie mchakato na uamuzi wa kuwafukuza uanachama na kisha itoe amri tatu.

Machi 10, 2023, Profesa Azaveri Lwaitama ambaye ni mjumbe wa bodi hiyo wakati akijibu maswali ya dodoso kutoka kwa jopo hilo, alidai kuwa Mdee na wenzake 18 wakitoka bungeni leo yeye atakuwa wa kwanza kuwatetea kurudishwa kwenye chama wakifuata utaratibu.

Alidai, Mwenyekiti Freeman Mbowe alikuwa akizungumza kumuita Mdee Nairobi, Kenya ili kuzungumza naye kwa kile ambacho wamekifanya kwa sababu yeye ndiyo alikuwa kiongozi wa wenzake kutokana na ushawishi mkubwa aliyokuwa nao.

Alidai kuwa Mbowe baada ya kuzungumza na Mdee, Mdee alilia, kwa hiyo kama watatoka leo bungeni yeye atakuwa mtu wa kwanza kuwatetea kurudishwa kwenye chama, kwa sababu shida sio ubunge wao, ni utaratibu haukufuatwa. "Utaratibu waliotumia ni batili na wakihuni kwa sababu haiwezekani mtu atoke gerezani usiku aghushi barua halafu aende akaapishwe hiyo sio sahihi kabisa," alidai Profesa Lwaitama.

"Hivi hata kama walipata matishio ya usalama wao kuwa kuna watu wataandamana, tufikirie tu enzi za Rais Dk. John Magufuli kuna mtu anaweza kufanya maandamano au ilikuwa janja janja yao tu," alidai Lwaitama.

Mdee na wenzake walifungua shauri hilo namba 36/2022 Julai 22, 2022 wakiomba mahakama hiyo ipitie mchakato na uamuzi wa kuwafukuza uanachama na kisha itoe amri tatu.

Katika shauri hilo, wabunge hao wanaiomba mahakama itengue mchakato na uamuzi wa kuwavua uanachama na pia iwalazimishe CHADEMA kuwapa haki ya kusikilizwa.

Pia, wanaomba amri ya zuio dhidi ya Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), kutokuchukua hatua yoyote hadi malalamiko yao yatakapotolewa uamuzi.

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Viongozi wa dini mnaaminiwa, mkionya mnasikilizwa

**VIONGOZI** wa dini ni watu wanaoaminiwa kwa kiasi kikubwa na waamini wao na wanapokemea jambo lolote ovu ni rahisi kuachwa.

Kwenye nyumba za ibada viongozi wa dini huchukuliwa na waamini wao kama watu waliotumwa na Mungu kuja kuwafundisha matendo mema na kuyafuata.

Kwa sababu hiyo, Waziri Mkuu, Kasim Majaliwa amewataka viongozi hao wasimamie haki na kuienzi kwa manufaa ya wananchi wa sasa na vizazi vijavyo.

Amewataka viongozi wa dini kukumbusha mara kwa mara waamini na watu wote kuhusu umuhimu wa kusimamia haki na kudumisha amani na kuiombea nchi na viongozi wake.

Rai hiyo ya Waziri Mkuu inakuja huku nchi ikiwa katika wimbi zito la binadamu kukiuka uumbaji wa Mungu na kwenda kinyume.

Wanaume sasa wanajigeuza na kuwa wanawake ili waolewe na wanaume wenzao na wanawake wanajigeuza na kutaka kuwa na misuli kama ya wanaume ili waweze kuoa wanawake wenzao.

Vitendo hivi vimeshamiri kutoka kwa watu wazima na sasa vinapelekwa kwa watoto ambao wanafundishwa kwenye baadhi ya shule, hali inayoleta hofu kubwa ya mporomoko wa maadili.

Serikali inachukua nafasi yake kukemea hali hii, taasisi mbalimbali zinakemea, lakini viongozi wa dini wana nafasi kubwa ya kukemea kwa sababu wanasikilizwa na wanaaminiwa kwa wanachokisema.

Kwenye nyumba za ibada iwe misikitini, kwenye makanisa iwe ajenda kwa viongozi hao kila wanapokutana na waamini wao kukaripia na kulaani.

Shule zinazofundisha watoto masuala dini nazo zina mchango mkubwa wa kukemea vitendo hivyo na walimu wanaogeuza shule hizo kuwa kichaka cha kuficha uovu wao hawana budi kuchukuliwa hatua kali.

Waziri Mkuu amewataka viongozi wa dini nchini kutochoka kufundisha na kulea vijana katika maadili mema na kuthamini kufanya kazi halali.

“Katika nyakati hizi ni ukweli ulio wazi kuwa kuna mmomonyoko mkubwa wa maadili katika jamii yetu, vitendo viovu na mambo yasiyompendeza mwenyezi Mungu yanazidi kuongezeka, mambo ambayo siku za nyuma yalikuwa nadra sana kutokea au kusikia, lakini sasa yanakuwa habari za kila siku na wakati mwingine huonekana eti ya kawaida,” anasema Majaliwa.

Kushuka kwa maadili ni jambo lenye athari mbaya kwa jamii na taifa kwa ujumla na kunachangia kurudisha nyuma juhudi za kujiletea maendeleo na kuifanya kazi ya kuondoa umaskini kuwa ngumu.

Anaamini kwa dhati kuwa viongozi wa serikali, dini na vyama vya siasa wakishika mafundisho ya dini na kuwa na hofu ya Mungu maovu mengi yatapungua na nchi kuongozwa vizuri.

“Naendelea kuwaomba kwa niaba ya serikali, viongozi wa dini zetu zote tusaidiane kuokoa taifa letu kimaadili na tuweke mkazo zaidi kwa vijana kwa sababu kwanza wao ndiyo wahanga wakuu wa maovu yanayotendeka, lakini pia wao ni taifa la leo na viongozi wa kesho.”

Waziri Mkuu pia alisisitizia suala la elimu na kueleza kuwa ni muhimu kwa maendeleo ya taifa lolote na kutaka viongozi wa dini kusaidia kuzungumza na wazazi na kuwaelimisha kuhusu umuhimu wa kusomesha watoto.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Halfani Chusi

## Muungwana Lazima Nilonge

# Wapiga debe stendi sasa wageuka kero

**WIMBI** la ongezeko la wapiga debe kwenye vituo vya mabasi linazidi kushika kasi, huku baadhi yao wakibadili dhana nzima ya kazi yao na kugeuka wezi.

Unapotaka kusafiri kwenda mkoa mwingine, unapofika kwenye kituo cha basi utakutana na wimbi la watu wanaotaka kujua wapi unaelekea, na wengine wanadiriki hata kupokonyana begi lako ili mradi apate ulaji ukikubali kupanda kwenye gari.

Ni biashara kweli, tunafahamu na wengine inawasaidia kuendesha familia zao, lakini kwa namna yoyote ile haipaswi kuwa kero kwa mteja anapofika kupata huduma ya usafiri.

Kuna haja ya serikali kuangalia namna nzuri ya kudhibiti wapiga debe, hawa ndio huwa chachu ya kupandisha bei kwa abiria ili apate cha juu wenyewe wanaita posho.

Ukikutana na mpigadebe njiani, pasi na kumuona muhusika wa gari, ni lazima bei itakuwa kinyume. Kwa mfano, nauli ya kwenda Dodoma ni Sh. 25,000, lakini mpiga debe atakwambia 30,000 ili apate chochote kitu.

Nadiriki kusema, huo ni sawa na wizi, haiwezekani umpokee abiria na umuongezee nauli, ili upate faida wakati mwenye gari huwa anawalipa kwa kazi ya kuita na kushawishi abiria kuingia kwenye gari husika.

Hata hivyo, bado wapiga debe hawa wamegeuka kero siku moja wakati ninasafiri kwenda Iringa, pale kituo cha basi cha Magufuli, nilishuhudia wapiga debe wakipokonyana begi la abiria mpaka likaharibika. Yote ni kugombea abiria bila ya utaratibu.

Wana kauli mbaya mdomoni, hata kama umeenda na mtoto kwa ajili ya kufuata usafiri, unaomba Mungu mmoja wao asiropoke.

Mavazi yao hayapo kikazi, hayajakaa katika staha inayotakiwa hujui mpiga debe yupi na kibaka ni yupi, wengine ni walevi kupitiliza unatamani hata asikuongeleshe maana mdomo wake haukushawishi kumjibu.

Kuna haja ya hili eneo kulitazama kwa umakini na kuliwekea mikakati thabiti itakayo kuwa rafiki kwa abiria wanapohitaji usafiri.

Sipingi, kama wakati mwingine wana umuhimu mkubwa kwa wale wasiojua wapi waelekee na usafiri wake unapatikana sehemu gani, lakini wanapaswa kuifanya kazi hiyo pasina kukera mteja.

Pia, tabia yao kuwapandishia bei abiria ikemewe, hii haijengi bali inabomoa na kuipa sifa mbaya sekta ya usafirishaji na wasafiri kwa ujumla wake.

Nakumbuka Rais Magufuli enzi za uhai wake, alisema hapendi kuona wapiga debe kwenye vituo vya mabasi na badala yake aliwataka wajiingize kwenye biashara ya ujasiriamali.

Kwa upekee, katika hili nampongeza sana Hayati aliona mbali alijua ipo siku watageuka kero kwa wasafiri na jamii kwa ujumla.

Kwa sababu ukiwaangalia wapiga debe wote ni vijana wenye nguvu, na uwezo wa kufanya kazi nyingine itakayowaingizia kipato badala ya kudanda danda vituoni.

Kwa mtazamo wangu, nadhani ni wakati sahihi sasa kuangalia namna ya kulijengea hoja hili suala na kuona namna ya kumaliza ghasia hiyo.

Tena kwa sasa teknolojia ipo juu sana, unaweza kukata tiketi hata kwa njia ya mtandao sasa fikilia umekata tiketi yako kwa njia hiyo, lakini bado unafika stendi ni vurugu tupu mpaka unapoingia kwenye gari.

Ukifikiria unapata jibu kwamba, hakuna maana ya kuwa na mfumo huo kama mazingira ya wapiga debe ambao muda mwingine wanageuka wezi kama alivyosema hayati Magufuli hayajadhibitiwa.

Lengo la abiria kukata tiketi kwa njia ya mtandao, inajumuisha pia, kuepuka ghasia hizo. Lakini, bado inaonekana sio dawa na ukimwambia mpiga debe kama umeshakata tiketi, anakuwa bado haelewi, atakuganda weee! Mpaka kwenye gari unaloingia ndipo anakuacha.

Hii sio kweli, haifai na haipendezi sidhani kama kuna abiria leo hii anaweza kutoka nyumbani kwake hajui anakwenda kupanda basi gani.

Wizara husika inapaswa kulingalia hili kwa macho matatu kuona namna bora ya kuliwekea mazingira mazuri, hata wageni wanapohitaji usafiri wanapokutana na hali hiyo wanaondoka na sifa mbaya kwa nchi yetu.

**Napatikana kwa simu: +255 787879707**

HABARI KITAIFA

# Dereva lori lililoua 13 na kujeruhi wawili anaswa

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

JESHI la Polisi mkoani Ruvuma limemkamata Thobias Njozi (47), mkazi wa Lizaboni, Manispaa ya Songea na dereva wa lori aina ya Fuso lililoanguka na kusababisha vifo vya watu 13 na majeruhi wawili kisha dereva kudaiwa kukimbia na kutokomea kusikojulikana.

Ilidaiwa kuwa lori hilo lilikuwa limesheheni mizigo na wafanyabiashara likitokea Kijiji cha Ndongosi likielekea katika mnada wa Kijiji cha Namatuhi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana ofisini kwake mjini hapa, Kamanda wa Polisi mkoani Ruvuma, Marco Chilya alisema askari polisi wa Idara ya Upelelezi tangu ilipotokea ajali hiyo Aprili 9 mwaka huu, waliendelea kufanya upelelezi wa kina na wamefanikiwa kumkamata Njozi akiwa kituo cha mabasi ya Kampuni ya Super Feo, ikidaiwa alikuwa anajiandaa kusafiri kwenda nje ya Mkoa wa Ruvuma.

Alikumbusha kuwa ajali ya gari hilo lenye namba za usajili T 800 BXB ilitokea Aprili 9 mwaka huu, eneo la Daraja la Mto Njoka, Kijiji cha Namatuhi kwenye barabara ya kutoka Ndongosi kwenda Namatuhi baada ya kupinduka na kusababisha vifo vya watu 13 na majeruhi wawili.

Alisema kuwa baada ya kutokea kwa ajali hiyo, dereva wa gari hilo alikimbia na kutokomea kusikojulikana.

Kamanda huyo alisema jeshi hilo liliendelea na msako na ilipotimu Aprili 16, majira ya asubuhi, katika ofisi za mabasi ya Kampuni ya Super Feo mkoani Ruvuma, walifanikiwa kumkamata Njozi ambaye alikuwa anajiandaa kusafiri.

Alisema kuwa katika mahojiano ya awali, polisi walibaini Njozi ni mmiliki wa gari hiyo lililopinduka na kusababisha vifo na majeruhi.

Alisema mtuhumiwa anatarajiwa kufikishwa mahakamani kwa hatua zaidi za kisheria mara tu uchunguzi wa ajali hiyo utakapokamilika.

Kamanda Chilya alisema majeruhi wawili wa ajali hiyo wanaendelea kuimarika kiafya na waliruhusiwa kutoka hospitalini walikokuwa wakipatiwa matibabu.

Alisema Jeshi la Polisi mkoani hapa linaendelea kuwasisitiza wananchi kuona umuhimu wa kufuata sheria na madereva wote wanapaswa kuhakikisha wanaendesha magari yao kwa kufuata sheria na kanuni za usalama barabarani.

Pia aliwaomba wananchi mkoani hapa kuendelea kushirikiana na Jeshi la Polisi kwa kutoa taarifa za uhalifu na wahalifu ili Mkoa wa Ruvuma uendelee kuwa na usalama kwa wakazi wote.

**Alisema kuwa baada ya kutokea kwa ajali hiyo, dereva wa gari hilo alikimbia na kutokomea kusikojulikana.**



Askofu Danstan Maboya akiwaombea baadhi ya washiriki wa kongamano la uamsho wa ndoa lililoandaliwa na Kanisa la Mlima wa Moto Mikocheni A, Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE.**

# OSHA yatoa hadhari nimonia mapafu meusi kwa wachimbaji

**Na Frank Monyo**

WAKALA wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) umewataka wawekezaji na waajiri katika makaa ya mawe kuzingatia ipasavyo sheria na miongozo ya usalama na afya ili kuwalinda wafanyakazi wao dhidi ya ajali na ugonjwa wa nimonia ya mapafu meusi unaoweza kuwapata katika maeneo yao ya kazi.

Meneja wa OSHA Kanda ya Kusini, Wilbert Ngowi alitoa rai hiyo alipohitimisha programu maalum ya siku nne ya mafunzo ya usalama na afya mahali pa kazi kwa viongozi na wafanyakazi wa sekta ya makaa ya mawe wilayani Mbinga mkoani Ruvuma.

"Sekta ya makaa ya mawe inakabiliwa na vihatarishi mbalimbali kama ilivyo kwa sekta zingine za madini. Mfano, mfanyakazi anapovuta vumbi la mkaa kwa muda mrefu anaweza kupata ugonjwa wa nimonia ya mapafu meusi (coal worker's pneumoconiosis), ugonjwa huu hauna dalili za haraka wala tiba, hivyo mfanyakazi akiathirika na huu ugonjwa utakuwa ndio ulemavu wake wa maisha na unaweza kumsababishia kifo.

"Hivyo basi, kutokana na sekta hii kukabiliwa na vihatarishi vingi na vinavyoweza kuhatarisha maisha ya wafanyakazi, tumeona tuanze kuchukua tahadhari mapema kwa kuendesha programu maalumu ya mafunzo kwa lengo la kuwapa elimu wafanyakazi hawa ili waepukane na vihatarishi hivi vya ajali na magonjwa vinavyoweza kuwapata katika maeneo yao ya kazi ikiwa ni pamoja na kuepukana na vumbi la makaa ya mawe.

"Nitoe wito kwa waajiri na wawekezaji katika makaa ya mawe wahakikishe kwamba wanazingatia taratibu zote za usalamaa na afya katika maeneo yao yote ya kazi kwa kuchukua tahadhari zote stahiki ikiwa ni pamoja na kuhakikisha vumbi linapungua katika maeneo yao pia wahakikishe vifaa vyote vinavyotumika katika shughuli mbalimbali vinamkinga mfanyakazi dhidi ya vihatarishi vya ajali na magonjwa," alisema.

Kupitia progamu hiyo ya mafunzo, Mkurugenzi wa Oparesheni wa Kampuni ya Uchimbaji wa Makaa ya Mawe ya Jitegemee Holdings, Boscow Mabena alieleza namna ambavyo kampuni hiyo imehamasika katika kuimarisha mifumo ya usalama na afya.

"Tunawashukuru sana OSHA kwa kutupatia elimu hii ya usalama na afya katika sekta yetu ya makaa ya mawe, wamekuwa wakitutembelea na kutupa miongozo mbalimbali ya namna sahihi ya kuboresha mazingira ya kazi.

"Hivyo, tumehamasika kwa kiasi kikubwa sana na tayari tumetenga bajeti ya mafunzo ya usalama na afya, tutapeleka wafanyakazi wakahudhurie mafunzo hayo yanayotolewa na OSHA," alisema Mabena.

Baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo kutoka kampuni mbalimbali, walieleza namna ambavyo elimu hiyo itawaongezea tija katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

"Nimeelimika kwa kiasi kikubwa sana na kama kiongozi itanisaidia kuwasimamia vyema wafanyakazi wenzangu katika eneo letu la kazi ikiwemo kuwalinda dhidi ya vumbi la makaa ya mawe linaloweza kusababisha ugonjwa wa nimonia ya mapafu meusi.

"Vilevile, tunaahidi kutekeleza mambo yote yaliyoagizwa na sheria ya usalama na afya ikiwamo kuhakikisha wafanyakazi wote wanatekeleza majukumu yao wakiwa wamevaa vifaa kinga," alisema Rajabu Miraji.

Merce Gerald, mhandisi kutoka Kampuni ya Jitegemee, alisema mafunzo hayo yataleta mabadiliko ya kiusalama kwa kiasi kikubwa katika maeneo yao ya kazi.

"Elimu hii itatusaidia sana kujikinga na vihatarishi mbalimbali tunavyokabiliana navyo katika maeneo yetu ya kazi, hivyo niombe OSHA waendelee kutoa mafunzo haya kwa migodi mingine ili waokoe maisha ya wafanyakazi wengine wa sekta hii," alisema.

KABWELA FADHILI MOHAMED



# Auawa akidaiwa mshirika kikundi cha Damu Chafu

**Na Neema Hussein,** MPANDA

MICHAEL Chapa (15), mkazi wa Mtaa wa Kivukoni, Manispaa ya Mpanda mkoani Katavi, anadaiwa kuuawa na wananchi wenye hasira kali, wakimtuhumu kuwa miongoni mwa kikundi kinachojihusisha na wizi na ubakaji, maarufu Damu Chafu.

Kikundi hicho kinahusishwa na matukio ya hivi karibuni ya wizi, uporaji wa simu, fedha, ubakaji na kujeruhi watu katika Kata ya Shanwe, hususani Mtaa wa Kivukoni.

Mtoto huyo alifikwa na umauti ikiwa ni siku chache tu baada ya mtu mmoja kuvamiwa na kukatwa sikio, huku washukiwa wakuu wakiwa ni kikundi hicho cha Damu Chafu.

Inadaiwa kuwa kutokana na kukithiri kwa matukio hayo, wananchi walianza msako dhidi ya vijana wanaounda kundi hilo la kihalifu.

Mashuhuda wa tukio hilo wanadai kuwa kabla ya kukamatwa kwa Michael na kupigwa hadi kuuawa, vijana wengine wawili walikamatwa na kushushiwa kipigo na wananchi, hata kufikia hatua ya kuwataja vijana wenzao wanaoshirikiana kufanya uhalifu mitaani.

Walidai kuwa siku iliyofuata, Michael alikamatwa na kushambuliwa kwa kutumia silaha za jadi hadi kusababisha kifo chake.

"Jana walipitishwa vijana wawili hapa, mmoja mdogo kabisa ana miaka kama tisa hivi wanapigwa kweli, yule mkubwa alikuwa anatema damu, walipowapiga wakawaacha.

"Leo tena ninatoka kwenye kazi zangu nikiwa na tenga langu la chainizi, ninaona watu wamejaa, ninauliza 'nini?', wanasema Damu Chafu anapigwa, kusogea namkuta bwana Michael kashapigwa, yuko hoi, kufikia saa nne naambiwa yule damu chafu aliyekuwa anapigwa kafariki," alidai Clement Pius

Titus Chapa, baba mzazi wa Michael, alisema alipigiwa simu akiwa shambani kuwa mwanawe anapigwa, hivyo awahi kwenda kumsaidia, lakini kutokana na kuwa mbali na eneo la tukio, hukuwahi na ilipotimu majira ya saa nne usiku, alitumiwa ujumbe mfupi kuwa mtoto wake amefariki dunia.

"Polisi walishawahi kuja nyumbani majira ya saa saba usiku na kuniuliza 'mwanao yuko wapi?', nikawajibu 'mimi sijui' na kweli hakuwamo ndani na sijui alipokuwa.

"Basi, walinikamata na kunipiga sana. Nilitoa Sh. 50,000 wakaniachia. Kijana wangu nimemsihi sana mimi na ndugu wengine kuwa aachane na hii kazi, kuna kipindi hadi nilimwambia twende shambani akagoma, hivyo mimi na wadogo zake na mama yake tukahamia shamba, yeye tukamwacha hapa, yaliyoendelea huku sijui hadi leo kuambiwa ameuliwa," alisimulia Chapa.

Mjumbe wa Mtaa wa Kivukoni, Kabambi Zacharia alikiri kutokea kwa mauaji hayo huku akidai vitendo vya uhalifu vimekithiri katika mtaa huo, akiwalaumu wazazi kutokutoa ushirikiano kwa viongozi ili kuwafichua vijana wahalifu.

Hivi karibuni, Jeshi la Polisi Mkoa wa Katavi liliwaarifu waandishi wa habari kuwa kupitia doria zake, liliwakamata vijana 15 na kuwafikisha mahakamani na baadhi kuachiwa kwa dhamana.




Mwanafunzi Shose Edwin (kushoto), akiwasilisha programu yao kwa majaji na wakufunzi (hawapo pichani), ambayo waliibuka washindi wakati wa mafunzo ya TEHAMA yaliyotolewa na Vodacom Tanzania Plc kwa kushirikiana na Tanzania Data Lab (dLab) kwa wanafunzi wa kike 65 kupitia programu yao ya 'Code Like a Girl' katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Ndaki ya Teknolojia za Habari na Mawasiliano (CoICT), mwishoni mwa wiki. Wanafunzi wa kike zaidi ya 1,700 wamewezeshwa na mafunzo mbalimbali ikiwemo 'coding' na kujengewa hamasa ya kupenda masomo ya sayansi, teknolojia, uhandisi, na hisabati (STEM). **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# DC, shekhe waipongeza Benki ya Exim kusaidia watu wenye uhitaji

**Na Mwandishi Wetu,** TANGA

BENKI ya Exim imehitimisha uandaaji wa futari kwa wateja wake katika mikoa mbalimbali nchini ikiwamo Dar es Salaam, Zanzibar, Dodoma na Tanga kwa msimu huu wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani huku wadau mbalimbali wa benki hiyo wakiwamo wateja, viongozi wa dini na serikali wakionyesha kuridhishwa na utaratibu wa benki hiyo wa kuwakumbuka watu wenye mahitaji maalum.

Katika kuhitimisha uandaaji wa futari hiyo mwishoni mwa wiki, viongozi waandamizi wa serikali na dini katika mikoa ya Tanga na Dodoma wakishirikiana na viongozi waandamizi wa benki hiyo waliongozwa na Ofisa Mtendaji Mkuu, Jaffari Matundu na Mkuu wa Rasilimali Watu, Fredrick Kanga waliungana na waumini wa dini ya Kiislamu katika mikoa hiyo kujumuika kwa ajili ya futari.

Kupitia kwa Mkuu wake wa Kitengo cha Hazina na Masoko ya Dunia, Nelson Kishanda, ilikabidhi msaada wa chakula na mahitaji muhimu kwa familia zenye uhitaji kupitia taasisi ya Maawal Islamic ya jijini Tanga, shughuli hiyo ikiongozwa na Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Hashim Mgandilwa aliyemwakilisha Mkuu wa Mkoa huo; na Shekhe wa Mkoa huo, Juma Luwuchu.

Viongozi hao; Mgandilwa na Shekhe Luwuchu, walionyesha kufuruhishwa na mtazamo wa benki hiyo wa kutoutazama Mwezi Mtukufu wa Ramadhani kama mwezi wa kujenga uhusiano na wateja wao pekee, bali pia kuutumia vyema mwezi huo kwa kuyakumbuka makundi yenye uhitaji bila kujali kama si wateja wa benki hiyo.

"Hiki kinachofanywa na Benki ya Exim ni mfano wa kuigwa. Wangeweza tu kukutana na wateja wao na kufuturu pamoja lakini wameona kitendo hicho pekee hakitoshi kuuheshimisha Mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani, hivyo wameona ni vyema wawakumbuke pia wenye uhitaji maalum.

"Kupitia Taasisi ya Maawal Islamic, wamekabidhi chakula kwa watu wenye uhitaji... hongereni sana," alipongeza Mgandilwa.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Exim, Jaffari Matundu alisema huo ni mwendelezo wa utaratibu wa benki hiyo kwa zaidi ya miaka 10 sasa wakilenga kujumuika na wateja wake kama hatua ya kuonyesha mshikamano na umoja katika kipindi cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Alisema benki hiyo inaheshimu sana Mwezi Mtukufu wa Ramadhani kutokana na ukweli kwamba ni kipindi ambacho mwanadamu anajiweka karibu na muumba wake kupitia mfungo na kufanya maombi.

"Kwetu sisi mwezi huu tunautazama kiimani zaidi ndio sababu tunazama makundi yote wakiwamo wateja wetu pamoja na watu wenye uhitaji maalum. Tumeweza kuandaa matukio kama haya mikoa mbalimbali ikiwamo Dar es Salaam, Zanzibar na leo tunakamilisha na mikoa ya Tanga na Dodoma.

"Zaidi tutaendelea kutoa zawadi za Sikukuu ya Eid al-Fitr katika maeneo mengine pia. Lengo ni wote tufurahie mwezi huu muhimu huku pia tukikumbushana kufanya kilicho chema mbele za Mungu wetu," alisema Matundu.

Hafla zote mbili zilihudhuriwa na wageni mbalimbali wakiwamo viongozi wa serikali, viongozi wa dini, viongozi wa vyama vya siasa, wateja, mawakala pamoja na wafanyakazi wa benki hiyo.

## Watalii 520 kutoka Israel waagwa wakiisifu Tanzania

**Na Lusungu Helela,** ARUSHA

ZAIDI ya watalii 520 kutoka Israel waliokuwa nchini kwa ajili ya kutembelea vivutio mbalimbali vya utalii, wameilezea Tanzania kuwa ni nchi pekee inayovutia kuitembelea kutokana na ukarimu wa watu wake ukiachilia mbali kuwapo wanyamapori na vitu vingine vingi vya asili.

Mwishoni mwa wiki iliyopita, mmoja wa watalii hao, Didace Alone, akiwa kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), alitoa pongezi hizo kwa Tanzania baada ya kuvitembelea vivutio mbalimbali akiongoza kundi hilo la watalii zaidi ya 520 kutoka Israel.

Alisema wameridhishwa na huduma za utalii zinazotolewa nchini na wanyamapori waliowaona mbugani na kuahidi kurejea tena wakati mwingine wakiwa wameambatana na ndugu, jamaa na marafiki ili kujionea upekee wa kutalii Tanzania.

Mtendaji Mkuu wa KIA, Christine Mwakatobe alisema kuwa tangu kuzinduliwa kwa filamu ya Tanzania The Royal Tour na mwongoza watalii namba moja nchini, Rais Samia Suluhu Hassan, watalii wamekuwa wakimiminika nchini kwa wingi. Easter Solomon,Ofisa Utalii Mwandamizi wa Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), alibainisha kuwa watalii kutoka Israel wamekuwa wanaitembelea mara kwa mara Tanzania kutembelea vivutio vya utalii kutokana na uhusiano mazuri baina ya nchi hizo mbili huku akisisitiza kuwa ukarimu wa Watanzania umekuwa chachu kwa watalii wa Israel kuichagua Tanzania.

Hilo ni kundi la nane kutoka Israel kutembelea Tanzania kwa mwaka huu pekee kujionea vivutio mbalimbali, raia wa nchi hiyo wakijiwekea utaratibu wa kuitembelea Tanzania angalau mara mbili kila mwaka.

Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2021/22-2025/26), pamoja na mambo mengine, umeelekezwa katika kuimarisha vivutio vya utalii ili vichangie zaidi kwenye Pato la Taifa na kutoa fursa za ajira.

Kwa mujibu wa mpango huo, ifikapo mwaka 2026, idadi ya watalii nchini inatarajiwa kufikia milioni tano na mapato ya dola bilioni sita kwa mwaka.

Vilevile, Programu ya Utalii ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ya 2020-30 inahimiza nchi wanachama wa jumuiya hiyo kuhakikisha kunakuwa na utalii endelevu na kuondosha vikwazo vya utalii na uhifadhi katika ukanda huo. Tanzania ni mwanachama mwasisi wa SADC.



# Waliofanya ufisadi KCBL kufikishwa mahakamani

**Na Mary Mosha** MOSHI

MRAJISI wa vyama vya ushirika nchini, Dk. Benson Ndiege amesema mtu yeyote aliyefanya ubadhirifu katika Benki ya Ushirika Kilimanjaro (KCBL), hatasalimika na kwamba watachukuliwa hatua za kisheria ikiwamo kurejesha fedha walizochukua.

Amesema kutetereka kwa benki hiyo kulichangiwa na baadhi ya watendaji wasio waaminifu huku akiwapongeza viongozi waliopo madarakani kwa kupata mafanikio ya kutoka kujiendesha kihasara hadi kuzalisha faida.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza na waandishi wa habari mkoani Kilimanjaro.

Dk. Ndiege alisema benki hiyo ilifika hatua ya kutaka kufungwa kutokana na kukosekana kwa watendaji waaminifu licha ya kupewa dhamana hiyo.

"Mwaka 2021/2022 benki hii imezalisha faida kubwa ya asilimia 25 kutoka Sh. bilioni nane hadi Sh. bilioni 11 ila bado watumishi waliosababisha hasara kwa kufanya ubadhirifu watachukuliwa hatua ikiwa ni pamoja na kulipa fedha za wanahisa,"alisema Dk. Ndiege.

Akizungumzia mafanikio hayo, Meneja wa KCBL, Godfrey Ng'urah alisema kwa mwaka wa fedha 2022 benki hiyo imekuza mtaji wa wanahisa kutoka Sh. bilioni 2.7 mwaka 2021 hadi Sh. bilioni 4.4 mwaka 2022.

"Mikopo kwa wateja imekuwa kwa asilimia 59 na kufikia Sh. bilioni 7.5 ukilinganisha na Sh. bilioni 4.7 ya mwaka 2021, amana za wateja zimekuwa kwa asilimia saba kutoka Sh.bilioni 5.5 za mwaka 2021, hadi Sh. bilioni 5.9 mwaka 2022, mapato ghafi ya Benki yameongezeka kwa asilimia 25 kufikia Sh.bilioni 1.5 toka Sh. milioni 1.2 ya mwaka 2021,"alisema.

Alisema pia imani kwa wateja imerejea na kumekuwepo na ongezeko la akaunti mpya zinazofanya miamala kwa wateja kufikia 21,000 kutoka 15,000 mwaka 2021.

Wakizungumzia upatikanaji wa faida katika benki hiyo, baadhi ya wateja akiwamo, Sembe Bwambo, alisema kwa sasa benki hiyo imeanza kuwa na mwelekeo na kuwataka wakulima kuendelea kununua hisa.

Mteja mwingine, Daud Mbazi alisema: "Kwenye benki hii ameona nguvu ya vyama vya ushirika na serikali, hivyo tuombe kwenye kila eneo ambalo lina ubadhirifu serikali ichukue hatua ili wanahisa wasipoteze haki zao na kukatishwa tamaa," alisema Daud Mbazi.

## Mchengerwa awaonya viongozi mradi wa REGROW

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Mohamed Mchengerwa amewaagiza wahusika wa Mradi wa Kuboresha Usimamizi wa Maliasili na Kukuza Utalii Kusini (REGROW), kuacha ukiritimba wakati wa utekelezaji wa mradi huo ili kukuza na kutangaza mazao mapya ya utalii katika mikoa ya kusini.

Alitoa agizo hilo juzi mkoani Arusha wakati wa hafla ya utiaji saini mikataba nane ya ujenzi wa miundombinu yenye thamani ya Sh. bilioni 157.29.

Mikataba hiyo imegawanyika katika makundi mawili ambayo ni mikataba ya ujenzi wa majengo pamoja na mikataba ya ujenzi wa viwanja vya ndege ambayo itatekelezwa katika Hifadhi ya Ruaha, Mikumi, Udzungwa na Nyerere na Msitu wa Asili wa Kilombero.

"Wanaopaswa kwenda kusimamia lazima waende wakasimamie na watendaji ambao watabainika kutofanya vizuri watachukuliwa hatua, dhamira ya serikali ni kuhakikisha kuwa tunafanya vizuri ili twende tukapate fedha zaidi katika awamu ya pili," alisema.

Aidha, aliwataka makandarasi wote waliosaini mikataba hiyo kutumia vizuri muda waliopewa kwa kufanya kazi nzuri katika muda mfupi na kwamba wasitarajie kuongezewa muda.

Mchengerwa alisema kwenye mikataba ya ujenzi wa viwanja inatarajiwa viwanja sita vya ndege kujengwa, kwamba viwanja vitatu vya ndege vitajengwa katika Hifadhi ya Ruaha, viwanha viwili katika Hifadhi ya Mikumi na Hifadhi ya Nyerere kitajengwa kiwanja kimoja cha ndege.


Aidha, aliswema katikaHhifadhi ya Udzungwa kutajengwa njia ya juu ya watalii ambayo inakadiriwa kuwa na kilomita moja ambayo inatarajiwa kuwa miongoni mwa njia ndefu zaidi Afrika Mashariki.

Mchengerwa alisema kuwa miundombinu mbalimbali kama vile majengo ya utalii, mageti, vituo vya habari, nyumba za watalii, hosteli vituo vya askari pamoja na maeneo ya kupumzikia yatajengwa ili kuhakikisha watalii wanafurahia wanapokuwa katika maeneo hayo.

Alisema ujenzi wa miradi hiyo itasaidia kufungua fursa na kukua kwa uchumi wa mikoa ya kusini, akiwaomba wakazi wa mikoa ya kusini kuchangamkia fursa wakati wa utekelezaji wa miradi.

Aidha, alitoa wito kwa wananchi wa mikoa ya kusini kuchangamkia fursa za ajira zitakazotokana na utekelezaji wa mikataba hiyo.

Katibu Mkuu wa Maliasili na Utalii, Dk. Hassan Abbasi, alisikitishwa na namna ambavyo mradi umekuwa ukishindwa kutekelezwa bila sababu za msingi, kwamba hadi Machi mwaka huu mradi huo ulikuwa umefikia asilimia 43.




Mtendaji Mkuu wa TANAPA, William Mwakalema (kulia), akiwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya China Henan International Cooperation Group Co. Ltd, iliyopewa zabuni ya kujenga kiwanja cha ndege katika Hifadhi ya Ruaha, Zhou Tao, wakionyesha mkataba wa makubaliano baada ya kutiliana saini, jijini Arusha jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Viongozi jumuiya za maji waagizwa kulinda vyanzo

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

SERIKALI wilayani Babati mkoani Manyara imewaagiza viongozi wa jumuiya za watumia maji kulinda na kutunza vyanzo vya maji ili Mwenge wa Uhuru utakapopita ukute viko salama.

Agizo hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki na Katibu Tawala wa Wilaya ya Babati, Halfani Mtipula, wakati akizungumza kwenye mkutano mkuu wa chombo cha watoa huduma ya maji ngazi ya jamii.

Mtipula alisema vyanzo vya maji visinatakiwa kulindwa na kutunzwa kwa kuwa bila vyanzo hivyo hakuna maji yatakayopatikana na uhai wa viumbe hai utakuwa hatarini kutoweka.

"Mhakikishe vyanzo vya maji vinalindwa na kutunzwa pamoja na miundombinu ya maji kwa kuwa vyanzo hivyo mwaka huu vitatembelewa na Mwenge wa Uhuru ili kuona namna vinavyolindwa,"alisema Mtapula.

Aidha, alisema kama kuna watu wamevamia vyanzo vya maji wanatakiwa kuondoka au kuondolewa ili kuvitunza vyanzo hivyo.

"Ni lazima mkusanye mapato na maofisa watendaji wa vijiji na kata tusaidiane kutafsiri sheria na baadhi ya mambo ili kuepusha malalamiko,"alisema

Kaimu Meneja wa Wakala wa Usambazaji wa Maji Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Babati, Fulgence Kalistus, alisema hali ya vyanzo vya maji ni ya kuridhisha isipokuwa kwenye vyanzo vya mtiririko ndiyo kuna matatizo ya uharibifu.

Alisema ili kuleta ufanisi kwenye utendaji wa jumuiya za watumia maji wameamua kutoa motisha kwa baadhi ya jumuiya ambapo miongoni mwa vigezo ni iwe imesajiliwa.

Alitaja kigezo kingine ni iwe na kamati tendaji inayofanya kazi vizuri, bila kusukumwa, iwe na skimu nyingi ambazo zinatoa huduma na iwe na mapato uwiano wake hauzidi matumizi.


Kaimu Meneja wa RUWASA mkoani Manyara, Amina Mwanja alizitangaza jumuiya zitakazopata motisha ni Jumuiya ya Boay Gidas ambayo inahudumia Kata ya Boay na Gidas na jumuiya nyingine ni Magara ambapo zilikabidhiwa pikipiki moja kwa ajili ya kuboresha utendaji wa kutoa huduma.

Mwenyekiti wa kamati ya watumia maji Kata ya Riroda, Ndege Qwaray, alisema ili kulinda vyanzo vya maji mtu akikamatwa anachunga mifugo faini Sh. 50,000.

Qwaray alisema mtu akiharibu miundombinu kwenye chanzo inafanyika tathimini ya miundombinu iliyoharibiwa na analipia fidia.

Alisema kikwazo wanachokabiliana nacho ni uelewa mdogo wa wananchi ambapo wanapoambiwa kulipia gharama za maji wanadai maji ni mali ya Mungu hawawezi kuyalipia.

Vile vile alisema katika kulinda vyanzo vya maji kila chanzo kwenye kijiji amewekwa mlinzi wa kudhibiti uharibifu.





# Viongozi wa dini waombwa kupambana ukiukwaji maadili

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme, amewaomba viongozi wa dini mkoani humo kupambana na tatizo la mmonyoko wa maadili kwa vijana.

Mndeme alibainisha hayo juzi wakati akifuturisha waumini wa Kiislamu mkoani Shinyanga, futari ambayo iliwashirikisha viongozi wa dini kutoka madhehebu ya Kikristo mkoani humo.

Alisema maadili ya vijana kwa sasa yameshuka ikiwamo kuiga mambo kutoka mataifa mengine na kufanya mambo ya hovyo, na kuwaomba viongozi wa dini kulikemea suala hilo.

Aidha, aliwaahidi viongozi hao kuwa serikali itaendelea kushirikiana nao katika nyanja mbalimbali hususani katika sekta ya afya, na elimu.

Pia, aliwaomba viongozi hao wasichoke kuendelea kuombea amani taifa, huku akiwasisitiza pia waumini wa dini ya Kiislamu kuutumia mfungo kuhakikisha wanawasaidia watu wenye uhitaji.

Shekhe wa Mkoa wa Shinyanga, Ismail Mkusanya, alisema kitendo alichokifanya Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga kufuturisha waumini wa dini ya Kiislamu ni kikubwa na dhawabu yake atalipwa na Mungu.

Alisema viongozi wa dini wataendelea kuliombea taifa ili liendelee kuwa na amani pamoja na kumuombea Rais Samia Suluhu Hassan awe na afya njema ili aendelee kuliongoza vyema taifa na kuwaletea maendeleo Watanzania.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Janeth Magomi akizungumza kwenye kampeni ya "kataa uhalifu" katika eneo linalopitiwa na mradi wa ujenzi wa Reli ya kisasa (SGR), kata ya Chibe, Manispaa ya Shinyanga juzi. **PICHA: MARCO MADUHU.**

## Mbunge awatangazia wananchi huduma ya maji bure

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MBUNGE wa Kahama, Jumanne Kishimba, amewatangazia neema wananchi wa kata ambazo zina upungufu wa upatikanaji wa maji kwamba wachote maji bure, atawalipia bili.



Alitangaza neema hiyo wiki iliyopita wakati akizungumza na wananchi wa Kata ya Mhungula Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga akisikiliza na kutatua kero mbalimbali za wananchi.

Alisema kata zilizopo pembezoni mwa mji wananchi wake wamekuwa wakitumia maji ambayo siyo safi na salama hali inayosababisha kuibuka kwa magonjwa ya mlipuko.

Hivyo, aliwatangazia wanawake kutoka Kata ya Nyahanga, Mhungula na Nyihogo watakuwa wanachota maji bure kila ifikapo siku ya Jumanne, kwamba atakwenda kulipa bili.

"Nafahamu mtandao wa maji ya Ziwa Victoria haujafika katika kata zote 20 hii ndiyo inanifanya mimi kutoa huduma hii kwa wananchi kupunguza adha ya upatikanaji wa huduma hii kwa wananchi," alisema Kishimba.

Baadhi ya wananchi walishukuru kwa kupokea huduma hiyo ambapo waliahidi kuitumia vyema kwa kutunza maji ya kutosha ili yawasaidie hususani katika siku ambazo siyo za kupata maji hayo.

Mmoja wa wakazi hao, Ester Bunzari alisema: "Hii huduma itatupunguzia adha ya kufuata maji umbali mrefu sambamba na kujikinga na magonjwa ya mlipuko yatokanayo na uchafu, kwani awali tulikuwa tukitumia maji ambayo hayakuwa salama".

# DC aagiza kuchunguzwa matumizi ya vitabu shuleni

**Na Vitus Audax,** ILEMELA

MKUU wa Wilaya ya Ilemela, Hassan Masala, amewaagiza maofisa elimu wote wilayani humo kuhakikisha wanachunguza matumizi ya vitabu vya ziada vinavyotumiwa katika shule binafsi pamoja na za serikali ili kudhibiti mmomonyoko wa maadili.

Alitoa agizo hilo juzi wakati akifungua kikao kazi cha Chama cha Walimu Tanzania (CWT) wilayani Ilemela mkoani Mwanza na kusema kuwa hali ya mmomonyoko wa maadili inatakiwa kudhibitiwa kuanzia shuleni.

"Vilevile nendeni kwenye shule zenu kwa kutazama vyema mienendo ya walimu wenu kutokana na baadhi ya walimu kukiuka miiko na kuanza kuchafua taaluma hii hatupo tayari kuendelea kuona hali ya unyanyasaji kijinsia shuleni" alisisitiza Masala.

Kadhalika, alisema msimamo wa serikali juu ya shule za bweni kufungwa uko palepale na hawatoruhusu kibali kwa shule yoyote kuendesha shughuli zozote zitakazowafanya wanafunzi kulala shuleni hususani wale wa elimu ya awali na msingi.

Kuhusu upungufu wa walimu katika maeneo mbalimbali ya shule wilayani Ilemela, alisema walimu wapo japokuwa mgawanyo haujakaa vizuri.

Hivyo alimtaka Ofisa Elimu wa Wilaya kwa kushirikiana na mkurugenzi kuhakikisha wanaangalia shule zenye walimu wengi na kuwapeleka katika shule zenye uhitaji wa walimu.

Akizungumza katika kikao hicho, Makamu wa Rais wa CWT, Suleiman Ikomba, aliwataka walimu wote kurudi katika mstari wa nidhamu na kuhakikisha wanafanya kazi kwa weledi na kurudisha heshima yao inayoharibiwa na baadhi ya walimu wasio waadilifu.

Awali akiwasilisha taarifa ya kikao kazi hicho, Katibu wa CWT Wilaya ya Ilemela, Asha Hussein alisema kikao hicho kililenga kutoa semina kwa viongozi wa ngazi mbalimbali za elimu pamoja na walimu katika kuhakikisha wanadhibiti migogoro kazini pamoja na kuhimiza ushirikiano kwa viongozi wa chama hicho pamoja na walimu wa ngazi mbalimbali.



Ukurasa 14

Jinsi akili bandia inavyokadiria na kutoa dawa kwa wagonjwa




Ukurasa 13

Walioelimika wafunguka magumu ya walivyokeketwa, yasiwakute wenzao

Nipashe
# TESA
Jumanne Aprili 18, 2023
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 12

Kijana Mhandisi Mario, aonyesha kwa vitendo, sasa amiliki kiwanda

ELIMU NA SABATO KASIKA

# Wenye sekta waorodhesha sababu za utoro kujiunga kidato cha kwanza

MIAKA ya hivi karibuni, kumeshuhudiwa kasi ya kuwapo hali ya baadhi ya wanafunzi wanaochaguliwa kuanza kidato cha kwanza kutoripoti katika shule walikochaguliwa, huku kukikosekana taarifa zinazohusu wao kutoripoti huko walikopangiwa.

Ni hali inayosababisha serikali za wilaya na mikoa katika maeneo hayo, nayo kuanzisha msako waliko waende shuleni kupata elimu.

Ni aina ya tabia inayochukua nafasi, vijana hawahudhurii katika shule walikochaguliwa, ilhali kunatolewa elimu bure, katika hitaji kuhakikisha kila mtoto anayechaguliwa huko, anapaswa kupata elimu hiyo.

Sasa imekuwa hali inayoshika kasi karibu mikoa yote na kusababisha serikali ichukue hatua ya kuanzisha msako dhidi yao. Nipashe imedadisi undani wake, kwa kuzungumza na wadau wa elimu, kupata undani wa mtazamo wao kuhusu utoro huo.

Dk. John Kalage ni Mkurugenzi wa Hakielimu ambaye anasema kuna sababu tatu zinazochangia kuwapo kwa utoro huo kila mwaka na kuifanya serikali ikaanzisha msako.

Mkurugenzi huyo anataja sababu ya kwanza kuwa ni baadhi ya wanafunzi na wazazi wao kutokuwa na mwamko wa elimu anayopaswa kupewa mtoto.

"Serikali imeongeza nafasi ya elimu ya sekondari hadi wanafaulu hata wale wasio na mwamko wa elimu, matokeo yake wanachaguliwa halafu hawaendi," anasema Dk. Kalaghe.



Mwalimu Mstaafu Suzan Lyimo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Anataja sababu ya pili, kuwa ni mfumo wa elimu, kwamba mwanafunzi anahitimu kidato cha nne au cha sita, anakuwa katika stadi za ujuzi, sawa na wa darasa la saba.

Dk. Kalage anafafanua hilo kwamba, mhitimu huyo wa darasa la juu, anahitimu katika ngazi hiyo bila ya kuwa na ujuzi wowote, anarudi mtaani kukaa kama wa darasa la saba na kwamba inakuwa ni hali inayomkatisha tamaa.

"Sababu ya tatu ni ugumu wa maisha. Wazazi wako tayari kuozesha binti zao au kuruhusu wakafanye kazi za ndani, ili wapate chochote cha kulisha familia, pia wanaruhusu watoto wao wa kiume kutafuta vibarua," anasema.

Dk. Kalaghe anaishauri serikali kubadili mfumo wa elimu, ili kila mwanafunzi anayehitimu ngazi ya elimu awe na ujuzi wa kumwezesha kujiajiri.

"Kwa sasa unakuta hata waliomaliza vyuo vikuu wakitafuta ajira, hawana ujuzi wowote. Nadhani mazingira hayo ya kuhitimu na kukaa vijiweni, yanaweza kusababisha baadhi ya wanafunzi kutoona umuhimu wa elimu, hivyo ni vyema mfumo wa elimu ukabadilishwa," anasema.

**UGUMU WA MAISHA**

Meshack Kapange, ni Katibu wa Chama cha Kutetea Haki na Masilahi ya Walimu Tanzania (CHAKAMWATA), anayetaja chanzo cha utoro huo, kuwa ni hali ngumu ya maisha kwa baadhi ya wazazi.

Kapange anasema, "Ukiangalia utagundua kuwa wanafunzi wengi watoro ni wa vijijini ambako wazazi wao wana uwezo mdogo wa kiuchumi," anasema Kapange.

Anafafanua, baada ya serikali kutangaza kutoa elimu bure, michango kuna lingine la upande wa pili limeibuka, kuwapo michango mingi shuleni, hata kusababisha wazazi washindwe kumudu gharama na kuwaacha watoto wao majumbani.

"Ninajua hadi sasa msako kwa ajili ya wanafunzi ambao hawajaripoti katika shule walizopangiwa unaendelea, ila ninaomba serikali iondoe michango, kwani imekuwa ni kikwazo," anasema.

Anasema, kila mwaka wanafunzi wa kidato cha kwanza wanatakiwa kuripoti kila mmoja akiwa na dawati, na kwamba wasio na uwezo kutengeneza dawati wanalazimika kubaki nyumbani.

"Ninadhani kusaka wanafunzi au wazazi wao na kuwaadhibu si vizuri, jambo la muhimu ni kutafuta chanzo cha utoro huo kwani kiko wazi," anasistiza, mwalimu, akilaumu kwamba katika nafsi yake haimuingii akilini, hali mwanafunzi anaposoma miaka saba katika elimu msingi, anafaulu kwenda sekondari halafu anaishia kubaki nyumbani.

"Hili anaweza kufanya mwanafunzi mmoja au wachache, lakini hili linahusisha wanafunzi wengi, kwani unakuta wamechaguliwa 400, lakini walioripoti shuleni 50 au 70 tu. Hapa kuna jambo, ninashauri lifuatiliwe," anasema.

**MAZINGIRA YA SHULE**

Mwalimu mstaafu wa Shule ya Sekondari Jangwani, Dar es Salaam, Suzan Lyimo, anadai chanzo cha yote ni mazingira ya shule nyingi za sekondari za kata, si rafiki kwa malezi ya wanafunzi.

"Unakuta mtoto anatembea umbali wa kilomita tisa hadi 10 kwenda shule, halafu shuleni kwenyewe hakuna walimu wa kutosha, hakuna vifaa vya kujifunzia na miundombinu ya shuleni ni mibovu," anasema Suzan.

Anaongeza kuwa wanafunzi wa kike wanakuwa katika mazingira hatarishi ya kubakwa kutokana na umbali wenyewe.

"Katika mazingira hayo, baadhi ya wazazi wanaona ni bora watoto wao wabaki nyumbani waendelee

INAENDELEA UK.12

ELIMU
NA CHRISTINA MWAKANGALE

ELIMU YA KUJIAJIRL...

# Kijana Mhandisi Mario aonyesha kwa vitendo, sasa amiliki kiwanda

"NILIPOMALIZA chuo nikaendeleza project (mradi wa andiko) ikawa biashara yangu, kuanzia mwaka 2016 mpaka 2020. Nilikuwa na hifadhi vifuu vya nazi kipindi chote. Hapo ndio wazo la kutengeneza 'carbon' kutoka kwenye kifuu cha nazi likaja"...

Ni kauli ya Tiberius Mario (33), Mhandisi Mhitimu wa Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam (UDSM), anayesema, anaishi katika alichokitarajia maishani, sasa anamiliki kiwanda cha kuchakata mafuta na vifuu vya nazi kwa ajili ya kuzalisha kemikali.

Akizungumza na Nipashe kwenye mazungumzo maalumu wiki hii, msomi huyo ambaye amezama katika stadi ya uhandisi kemikali, anasema tangu akiwa masomoni alipanga kujiajiri na kuajiri, na ndicho kilichopo sasa.

Sasa Mhandisi Tiberius, ana Tuzo ya Taifa ya Mbunifu Bora ya Mwaka 2022, akisema sasa anaangalia soko la kimataifa kuuza bidhaa zake. Fuatilia mazungumzo yake na mwandishi wa makala hii:

***Swali: Kwanza kwanini ulikuja na wazo la mradi huu? Ulihifadhi vifuu kiasi gani kwa miaka minne?***

***Jibu:*** Nilipomaliza chuo nikaendeleza hiyo 'project' (mradi) ikawa biashara yangu, kuanzia 2016 mpaka 2020 nilikuwa nahifadhi vifuu vya nazi, kipindi chote. Hapo ndio wazo la kutengeneza 'carbon' kutoka kwenye kifuu cha nazi likaja.

Mradi wa mafuta ya nazi nilianza mwaka 2016, lakini mradi wa 'activated carbon; nilianza 2020 kama research (utafiti), nikaenda mpaka 2022, nikaanza kuzalisha baada ya kuwa mshindi wa kwanza MAKISATU.

Miaka minne nilipata kama tani 20 hivi. Nilikuwa nakusanya kila ninavyofanya 'process' (mchakato) za mafuta. Lakini, nilipoanza mradi nilikusanya mitaani kwa muda mfupi na nilipata tani 12 ndani ya wiki moja. Vifuu vipo vingi.

Niliona kuna fursa, kwa sababu Tanzania tunaagiza nje tani zaidi ya 1,530 za carbon. Tanzania kwa mwaka tuna uwezo wa kuzalisha nazi milioni 800. Mafuta mwali ya nazi (edible oil) kwa lita zinatumika nazi kati ya 15 hadi 18.

Maana yake kwa mwaka tukisema hizo nazi tuchukue nusu tu tuzalishie mafuta zingine tuwaachie ndugu zetu wapikie tunaweza kupata lita zaidi ya 30,000. Na hapo hujazungumzia 'coconut husk (maganda)' 'coconut flour' (ini lake)' na coconut shells (ganda kuu) ambazo nazo zina mambo yake.

***Swali: Je, ulianza lini huo mradi?***

***Jibu:*** Mwaka 2015 nilikuwa mwaka wa nne Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, uzalishaji wa mafuta ya nazi ilikuwa ni 'project' (andiko la mradi) yangu ya mwaka wa nne.

***Swali: Umeshapata matokeo chanya, kwa maana ya soko, Je umelisajili wazo lako?***

***Jibu:*** Nimekwisha supply (sambaza) Chunya mkoani Mbeya, Shelui huko Singida na Ushirombo Katente (kituo cha mfano cha Stamico). Wazo langu nimelisajili.

***Swali: Na vifuu hivyo hasa ni kwa ajili ya shughuli gani? Kwa lugha rahisi.***

***Jibu:*** Vifuu hivi ni kwa ajili ya uzalishaji wa activated carbon. Inatumika kunasia dhahabu migodini na kupunguza chlorine iliyozidi kwenye maji.

***Swali: Malighafi unapata wapi, Je, hazina ugumu wa kupatikana na iwapo unanunua vifuu kilo moja au ujazo upi na unanunua kwa shilingi ngapi?***

***Jibu:*** Malighafi napata kwenye masoko ya Ilala, Stereo, Temeke na Kinondoni. Lakini, pia watu wanakusanyia wanniletea. Nanunua kiroba kikubwa kwa Sh 4,000 hadi 6,000.

***Swali: Umeajiri watu wangapi rasmi na vibarua?***

***Jibu:*** Watu rasmi niliowaajiri wapo watano na vibarua wanafika mpaka saba.

***Swali: Kiwanda chako kiko wapi?***

***Jibu:*** Kiwanda changu kiko Goba Mpakani, hapa Dar es Salaam.

***Swali: Changamoto unazozipitia ni zipi kwenye kazi zako?***

***Jibu:*** Kwanza vifaa vyangu vinanipa volume chache, changamoto ni mitambo mikubwa ya carbonizer (cha kuchomea vifuu), 'crusher' (kutengenezea chenga) na 'activator' kubwa. Niliyo nayo ni ndogo yenye uwezo wa kilogramu 100 kwa siku.

***Swali: Je, kama kijana unachokiishi sasa ndicho ulichokiwaza awali kwa maana kujiajiri, yaani ulitarajia uje kuwa nani?***

***Jibu:*** Mimi ni mhandisi wa kemikali toka nimemaliza niliamua kujiajiri ndio maana nikatoka na project (mradi) yangu ya mafuta ya nazi nilianza nayo na sasa nipo kwenye 'project' ya pili ya kutengeneza activated 'carbon' kwenye kifuu cha nazi. Ninachokifanya nakiishi na ndio dream (ndoto) yangu.

***Swali: Una wito gani kwa vijana kujiajiri na serikali hasa (wa wabunifu kama wewe?***

***Jibu:*** Wito wangu ni vijana tusipuuze projects (miradi) zetu za chuo hasa hizi zilizokaa kijasiriamali. Serikali ituangalie sisi wabunifu projects zetu zikiwezeshwa zinaweza kufanya vizuri sana. Kwa mfano, kwa Tanzania hatuna kiwanda cha carbon, mimi ndio wa kwanza kukianzisha. Serikali inishike mkono tutengeneze kiwanda hapa Tanzania.



Mhandisi Tiberius Mario, akiwa kwenye shughuli za ubinifu wake uliomwajiri. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

> "Kwa mfano, kwa Tanzania hatuna kiwanda cha carbon, mimi ndio wa kwanza kukianzisha. Serikali inishike mkono tutengeneze kiwanda hapa Tanzania.

## Wenye sekta waorodhesha sababu za utoro kujiunga kidato cha kwanza

**INATOKA UK.11**

na mambo mengine kuliko kuwapeleka katika hatari," anasema.

Aidha, anasema wanafunzi wengine wanaacha kuendelea na masomo ya sekondari, kwa madai kwamba haiwasaidii lolote na kwamba wanaamua kujishughulisha na biashara mbalimbali, ili kujiandalia maisha ya baadaye.

"Kiukweli ni kwamba hakuna ajira, hivyo wanaona hata wakisoma ni sawa na kupoteza muda, hasa wanapowaona wenzao ambao hawajasoma wamefanikiwa, nao wanaona ni bora wajiingize kwenye biashara," anasema.

Hata hivyo, anasema pamoja na changamoto zote, anahimiza kuwa elimu ni muhimu kwao na daima isipuuzwe, badala yake ithaminiwe na kila mtu.

Anashauri kwamba, ni muhimu kwa serikali ikaboresha miundombinu ya shule zake ziwe rafiki kwa wanafunzi, ili kuondokana na adha ya wanafunzui kwenda shule hadi wanaposakwa kila mwaka, kwa wale wasiohudhuria masomo.

ELIMU

NA JALIWASON JASSON,
ALIYEKUWA TARIME

SIRI KUU ILIKOJIKITA KWA WAKAZI WA TARIME;

# Walioelimika wafunguka magumu ya walivyokeketwa, yasiwakute wenzao

NI hatua ya mageuzi, elimu stahiki ikichukua nafasi yake, sasa waathirika wanaanza kupaza sauti ya kutoa kilio kwa vyombo vinavyohusika vichukue hatua stahiki, kuwanusuru na mikasa wanayopitia kukumbana na adha ya ukeketaji.

Binti (jina limehifadhiwa) kutoka kabila la Wakurya mkazi wa Borega kata ya Mbogi wilayani Tarime, ambaye ni mwathirika wa ukeketwaji angali katika umri wa miaka 14, anasema alikeketwa kunusuru ndoa ya mama yake mzazi iliyokuwa hatarini kuvunjika, endapo asingepitia hatua hiyo, ingekuwa mwisho wa ndoa ya mama yake.

Binti huyo anaeleza kuwa, baada ya kukeketwa mwaka 1999, akabahatika kupata mchumba na kuolewa akiwa na umri mdogo na ndoa yake haikudumu kutokana na kile alichosema halikuwa chaguo lake, bali alilazimishwa kuolewa baada tu ya kukeketwa.

"Mimi kama mwanamke sasa najitambua na nimepata elimu ya madhara ya ukeketaji kupitia elimu makanisa, elimu shuleni, taasisi mbalimbali zikitoa elimu ya madhara ya ukeketaji, serikali pamoja na makongamano ya hadhara.

"Kwa hali hiyo, natumia elimu niliyoipata kuwanusuru wasichana ambao wanataka kufanyiwa vitendo kama hivyo kuwa vina madhara kiafya na kijamii. Kwa hali hiyo, waachane na wasome na wataolewa na vijana walioelimika," anaeleza.

Mwanamke huyo anasimulia kuwa ameshuhudia wasichana walio wengi wamekeketwa wakitoka kwenye ndoa zao, kwa sababu wanapokuwa na waume zao hawana hisia za kimapenzi, kutokana na kulazimishwa kuolewa.

Anafafanua kwamba mabintui hao wapokutana na wapenzi wapya, wanaamua kutupa ndoa ya zamani, walikoolewa kwa lazima, hata wako kwa miaka mingi.

"Waliokeketwa hisia za kimapenzi zipo mbali wakati wa tendo la ndoa kutokana na kuondolewa kiungo cha hisia, tofauti na wasichana ambao hawajafanyiwa vitendo vya ukeketaji.

"Kiungo kilichotolewa mwilini ni cha thamani sana... unapoondoa unasababisha kutokea madhara ambayo hayatarajiwi kutokea. Kwa mtu kama mimi niliyekeketwa, nachelewa kupata hisia za kimapenzi wakati wa tendo, jambo ambalo linasababisha kutafuta michepuko wapya, ili kuona kama itasaidia mimi kujisikia tofauti. Hiyo ni hatari kwa dunia ya sasa ya magonjwa," anasema.




Harakati za kupambana na ukeketaji wilayani Tarime, inayoendana na elimu kwa umma. **PICHA: MAKTABA.**

Mwanamke huyo anataja madhara mengine kwa waliokeketwa, ni pamoja na kuonekana umri mkubwa kwa msichana aliyekeketwa, ukilinganishwa na umri wake wa kuzaliwa na hata kulinganisha na ambaye hajafanyiwa vitendo hivyo.

Pia, anataja madhara ya binti aliyekeketwa anajenga tabia ya kiburi, akijihisi ni 'mwanamke kamili', ilhali umri wake huenda bado ni mdogo.

Ligine analoshauri ni kutaka elimu iendelee kutolewa kwa ufasaha kwa wahusika kama vile wazee wa mila mang'ariba vijana wa kike na kiume, wazazi na walezi, huku wakiwezeshwa kupata mahitaji muhimu waondokane na dhana ya tamaa ya kuwatumia watoto wa kike kama eneo na sehemu ya kupatia mitaji.

**NDOTO ZINAHARIBIWA**

Binti (jina tunalo) kutoka kata ya Binagi, wilaya ya Tarime, mwenye umri wa miaka 24, ana simulizi yake akionyesha hisia za uchungu kwamba, mila za jamii yake zilivyompa majukumu akiwa yungali mdogo na kumsababishia maisha magumu.

Anasema, kwa sasa anaishi na mume wake iliko familia ya mwanaume huyo akibebeshwa jukumu la kuwa, mlezi mkuu wao na wakati huohuo ni mzazi mahali hapo, akiendeleza ukoo huo.

Mama huyo kijana, anatamka kwa sasa ana umri wa miaka wa ujana, ni mama wa watoto wawili wa kike, wenye umri wa miaka minane na mitano.

Anasema, mara baada ya kuolewa kuepuka mateso kutozaa kama ilivyowakuta mabinti wengine, anataja chanzo cha yeye kuolewa mapema ni kwa sababu ya ukeketaji ni mila za jamii yao, elimu ndogo ya wazazi, nguvu za giza na umasikini.

"Maisha yangu yote yamekuwa yakiamuliwa na wazazi kuanzia mdogo hadi nilipofika sikuwahi kupata nafasi ya kuchagua maisha yangu, nililazimishwa kukeketwa na kuolewa wazazi wangu wakidhani mahari itawatajirisha, lakini bado maisha ni magumu kama zamani na wameshaniozesha.

"Mimi sina uwezo sana kwasababu sijasoma nategemea kilimo cha kazi ngumu kulisha watoto wangu na mume wangu. Kila mmoja kwa nafasi yake, jamii inatakiwa kuungana kwa pamoja na kuwanusuru watoto wa kike kutokana na janga la ukeketaji.

"Mimi nisingekeketwa na kuolewa, ningekuwa na kazi niliyosomea, lakini kwa sababu jamii yangu haitaki wasichana tusome, wanahimiza mila tu na sio elimu na kutusababishia maisha magumu tusiyoyapenda na hata wao, pia hatuwezi kuwasaidia kutoka katika umasikini," anafafanua.

> "Mimi sina uwezo sana kwasababu sijasoma nategemea kilimo cha kazi ngumu kulisha watoto wangu na mume wangu.

Anafafanua kuwa, hata mazingira yanayotumika kuketeta siyo salama, licha ya kuwapo ng'ariba, kila mmoja huja na wembe wake, katika eneo ambako pia haparidhishi, bali wanachojali ni ukusanyanji pesa.

Kimsingi, analalamika, kuwa ni eneo liko mahsusi katika ukusanyaji pesa na halifanyiwi usafi au halikaguliwi na bwana afya wa kiserikali, katika kumuosha mhusika aliyekeketwa.

Inaelezwa, kazi hiyo inafanyika pasipo kutumika sindano ya ganzi, anayekeletwa anapata maumivu, damu inaganda kwenye kidonda na mazingira mengine magumu kuelezwa, zikitawaliwa na harufu mbaya hata kidonda kikipona.

Rai yake sasa mama huyo kijiana, ni kwamba elimu iendelee kutolewa kuhusi ya madhara ya ukeketaji na ukatili kwa wanawake, pia watoto wakemewe kwa tabia ya kutembea na makundi rika yasiyo na nidhamu ya kizalendo, ikwafikie pia wazee wa mila na waganga wa jadi wanaohausika nayo.

Pia, ana msisitizo kwamba, haja ya elimu kutolewa pale familia inakataa kumfanyia mtoto ukeketaji, hata kutumia vitoshio vya namna mbalimbali ikiwamo 'nguvu za giza' ili wanaokaidi waogope.

**TABIBU AFAFANUA**

Tabibu Bingwa wa Wanawake, Dk. Catherine Magari kutoka Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara, akiwakilisha wataalamu wa afya, anaeleza namna ukeketaji ulivyo na madhara kwa mwanamke, hasa anapojifungua humsababishia kovu la kudumu.

ELIMU
NA MWANDISHI WETU

# Jinsi akili bandia inavyokadiria na kutoa dawa kwa wagonjwa

Ni aina yake, pale Dk Talia Cohen Solal, anatumia AI kumsaidia yeye na timu yake kupata dawa bora za mfadhaiko kwa wagonjwa.

Daktari huyo ameketi chini kwenye darubini ili kutazama kwa makini seli za ubongo wa binadamu zinazokuzwa kwenye sahani maalum ya kuchunguza vijidudu.

"Ubongo unahitaji makini, mgumu na mzuri," anasema, mwanasayansi wa neva, Dk Cohen Solal ndiye mwanzilishi Mwenza na Mtendaji Mkuu wa kampuni ya teknolojia ya afya ya Israeli Genetika+, iliyoanzishwa mwaka wa 2018.

Ni kampuni anayosema, teknolojia yake inaweza kulinganisha vyema dawa za mfadhaiko na wagonjwa, ili kuepusha athari zisizohitajika, na kuhakikisha kuwa dawa iliyowekwa inafanya kazi vizuri iwezekanavyo.

"Tunaweza kuainisha dawa zinazofaa kwa kila mgonjwa mara ya kwanza," anaongeza Dk. Cohen Solal.

Kamuni Genetika+ hufanya hivi kwa kuchanganya teknolojia ya hivi punde zaidi katika seli shina, ukuaji wa seli mahususi za binadamu, na programu ya akili ya bandia (AI).

Kutokana na sampuli ya damu ya mgonjwa mafundi wake wanaweza kuzalisha seli za ubongo. Hizi, huwekwa wazi kwa dawa mfadhaiko kadhaa na kurekodiwa kwa mabadiliko ya seli inayoitwa 'biomarkers.

Habari hiyo inapochukuliwa pamoja na historia ya matibabu ya mgonjwa na data ya kijeni, kisha huchakatwa na mfumo wa AI ili kubaini dawa bora, ambayo daktari anaweza kuagiza na kipimo.



Dk Talia Cohen Solal (kushoto), akiwa na timu yake kazini. **PICHA: NEEMA HUSSEIN**

Ingawa teknolojia hiyo kwa sasa bado iko katika hatua ya maendeleo, Genetika+ yenye makao yake jijini Tel Aviv, Israel inakusudia kuzindua kibiashara mwaka ujao.

Mfano wa jinsi AI inavyozidi kutumika katika sekta ya dawa, kampuni imepata ufadhili kutoka kwa Baraza la Utafiti la Umoja wa Ulaya na Baraza la Ubunifu la Ulaya.

Genetika+ pia inafanya kazi na kampuni za dawa kuunda dawa mpya za usahihi. Kwa sasa, kampuni inatarajia kazi yake itakuwa katika mahitaji makubwa katika siku zijazo. Kuna zaidi ya watu milioni 280 duniani kote ambao wanakabiliwa na unyogovu, kulingana na Shirika la Afya Duniani.

Na ingawa kuchukua dawa mfadhaiko, hakika inatajwa haitakuwa tiba sahihi kwa wote, imekadiriwa kwa muda mrefu kwamba karibu theluthi mbili ya maagizo ya awali ya mfadhaiko au wasiwasi huenda yasifanye kazi ipasavyo.

"Tuko katika wakati mwafaka kuweza kuchanganya teknolojia ya kisasa ya kompyuta na maendeleo ya teknolojia ya kibaolojia," anasema Dk. Cohen Solal.

Mhadhiri Mkuu wa matibabu na sayansi ya data katika Chuo cha King's London, Uingereza, anasema AI anakotumikia hadi sasa imesaidia kwa kila kitu 'kuanzia kutambua jeni linaloweza kulenga kutibu ugonjwa fulani na kugundua dawa mpya, kuboresha matibabu ya wagonjwa.

Anadems, kuna utabiri mkakati bora wa matibabu, kugundua alama za viumbe kwa matibabu ya kibinafsi ya mgonjwa, au hata kuzuia ugonjwa huo kupitia utambuzi wa mapema wa dalili za kutokea kwake".

Bado mtaalamu mwenzake wa AI Calum Chace anasema kwamba, kuchukua AI katika sekta ya dawa bado ni "mchakato wa polepole".

"Kampuni za dawa ni kubwa, na mabadiliko yoyote makubwa katika jinsi ya kufanya utafiti na maendeleo yataathiri watu wengi katika tarafa tofauti," anasema Chace, ambaye ni mwandishi wa vitabu kadhaa kuhusu AI.

"Kuwafanya watu hawa wote wakubaliane na njia mpya ya kufanya mambo ni ngumu, kwa sababu walio waandamizi walifika hapo walipo kwa kufanya mambo kwa njia ya zamani.

"Wanafahamu hilo, na wanaliamini. Wanaweza kuhofia kuwa na thamani ndogo kwa kampuni kama kile wanachojua kufanya ghafla kitapungua thamani."

Hata hivyo, Dk Sailem anasisitiza, sekta ya dawa haipaswi kujaribiwa kusonga mbele na AI, na inapaswa kutumia hatua kali kabla ya kutegemea utabiri wake.

"Mtindo wa AI unaweza kujifunza jibu sahihi kwa sababu zisizo sahihi na ni jukumu la watafiti na watengenezaji kuhakikisha kuwa hatua mbalimbali zinatumika ili kuepusha upendeleo, haswa wakati wa mafunzo juu ya data ya wagonjwa," anasema.

Kampuni ya dawa ya Insilico yenye makao yake Hong Kong inatumia AI ili kuharakisha ugunduzi wa dawa.

"Jukwaa letu la AI lina uwezo wa kutambua dawa zilizopo ambazo zinaweza kutumika tena, kubuni dawa mpya kwa malengo ya magonjwa yanayojulikana, au kutafuta shabaha mpya kabisa na kubuni molekuli mpya," anasema mwanzilishi mwenza na mtendaji mkuu Alex Zhavoronkov.

Dawa yake iliyotengenezwa zaidi, matibabu ya hali ya mapafu inayoitwa 'idiopathic pulmonary fibrosis', sasa inajaribiwa kimatibabu.

Mtaalamu Zhavoronkov, anasema kwa kawaida huchukua miaka minne kwa dawa mpya kufikia hatua hiyo, lakini anaipongeza shukrani kwa AI, kampuni ya Insilico Medicine imefanikisha "ndani ya miezi 18, kwa sehemu ndogo ya gharama".

Anaongeza kuwa kampuni hiyo ina dawa nyingine 31 katika hatua mbalimbali za maendeleo.

Huko Israeli, Dk Cohen Solal anasema AI inaweza kusaidia "kutatua fumbo" la dawa gani hufanya kazi.

• *Kwa mujibu wa BBC*

## WANENAVYO MALENGA

### NINI UNACHOJILISHA?

1. Nini unachojilisha, katika yako maisha,
Hicho hakiwezi isha, kitavyokuhangaisha,
Habari zinazochosha, kichwani kwako safisha,
Soma hayo hovyo hovyo, nawe uwe ni wa hovyo.

2. Masikio sikilisha, ya kinyaa ya kuchosha,
Usidhani wayafisha, kwako wayaimarisha,
Ndiyo yatajirudisha, kwako kujimilikisha,
Sikiza sana ya hovyo, nawe uwe ni wa hovyo.

3. Macho wayatazamisha, yale yanasikitisha,
Unarudisharudisha, eti dunia yaisha,
Ndivyo unajirandisha, mwilini yatakutosha,
Tazama vitu vya hovyo, nawe uwe ni wa hovyo.

4. Mizaha ukidumisha, na hata kujisemesha,
Kwako takuwa maisha, mwili kuufurahisha,
Kule itakufikisha, kule umejilowesha,
Penda mizaha ya hovyo, nawe uwe ni wa hovyo.

5. Mkono ukikukosesha, ukate uweze kwisha,
Macho yakulazimisha, geuka kuyazimisha,
Miguu kupelekesha, njia yako badilisha,
Fanyafanya mambo hovyo, nawe uwe ni wa hovyo.

6. Dhambi unazisemesha, tangaza kama tamasha,
Unadhani zitakwisha, pengine wazivumisha,
Wengine wawaamsha, waweze kujaribisha,
Fanyafanya mambo hovyo, nawe uwe ni wa hovyo.

7. Neno linatukumbusha, kwamba mizaha yatosha,
Huko kujitambulisha, ni ligi unaanzisha,
Itayagusa maisha, ndiyo hivyo unakwisha,
Fanyafanya mambo hovyo, nawe uwe ni wa hovyo.

8. Vitabu vinaonesha, tangu zama za maisha,
Dhambi tunazoonesha, huko waliharamisha,
Lakini hazijaisha, sawa na yetu maisha,
Fanyafanya mambo hovyo, nawe uwe ni wa hovyo.

9. Kile tungekizidisha, ni watoto kufundisha,
Kizazi kisije kwisha, kwingine liwe tamasha,
Mungu hasa atutosha, kwa mwongozo wa maisha,
Fanyafanya mambo hovyo, nawe uwe ni wa hovyo.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**



## Vodacom yaja na ‘zaidi ya mtandao’ kwa wateja wake

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KAMPUNI ya Vodacom Tanzania imezindua kampeni mpya ijulikanayo ‘zaidi ya mtandao’ ambayo itawezesha wateja wake kutuma na kutoa pesa bila ya tozo kwa miamala chini ya Sh. 50,000.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi wa Biashara na Masoko wa kampuni hiyo, Brigita Shirima alisema kuwa kampeni hiyo ni mwendelezo wa namna ambavyo kampuni hiyo inagusa maisha ya Watanzania.

Alisema kampeni hiyo inahamasisha Watanzania kujiunga na mtandao wa Vodacom ulioenea nchi nzima na wenye kasi ya 5G.

Alisema wateja watafurahia vifurushi vya bei nafuu na huduma kemkemu za M-Pesa.

Alitaja baadhi ya faida kwa mteja mpya wa mtandao wa Vodacom ni kurudishiwa asilimia 15 ya gharama za bando pindi akinunua vifurushi kupitia M-Pesa.

Aliongeza kuwa Vodacom Tanzania inajivunia kuendelea kuboresha mtandao wake ambapo Septemba mwaka jana walizindua huduma ya 5G yenye ubora, ufanisi na iliyoenea nchi nzima kwa shughuli binafsi na za kibiashara.

Aidham alielezea sababu moja wapo inayoifanya Vodacom kuwa ‘zaidi ya mtandao’ ni kwamba mpaka sasa ina mawakala wa mauzo takribani 29,000 walioenea nchini kuwahudumia Watanzania.

Mkuu wa Kanda ya Kaskazini wa kampuni hiyo, George Venanty, alisema uzinduzi wa kampeni hiyo umefanyika kwa pamoja katika kanda nyingine nne tofauti.

Alizitaja kuwa ni Kanda ya Ziwa, Kanda ya Dar es Salaam, Kanda ya Kati na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, kwamba shughuli mbalimbali zitaendelea na kuenea sehemu zingine.

Alisema kampuni hiyo inaamini kwamba washirika na wadau wake waliotapakaa nchini wataendelea kuwaunga mkono kupitia ushirikiano walionao kwa miaka mingi katika kuhakikisha Watanzania wanafikiwa na huduma bora na nafuu za mawasiliano.

# Mwekezaji amwangukia Rais Samia madai kupokwa ardhi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MFANYABIASHARA mzawa, Leonard Suih, aliyewekeza mkoani Singida, amemuomba Rais Samia Suluhu Hassan, kuingilia kati mgogoro kati yake na Halmashauri ya Manispaa ya Singida uliodumu kwa zaidi ya miaka 28.

Akizungumza na waandishi wa habari mkoani hapa, Suih alisema uongozi wa Manispaa ya Singida unataka kumuondoa eneo alipojenga vitega uchumi vyake ikiwamo majengo ya biashara yenye thamani ya Sh. milioni 700.

Alisema mgogoro huo umekuwa ukiibuka na kupoa mara kwa mara hali ambayo inasababisha ashindwe kutekeleza majukumu yake kwa amani na kumwathiri kisaikolojia.

Suih alisema miaka 28 iliyopita alipatiwa eneo na Manispaa ya Singida ambalo lilikuwa dampo katika stendi ya mabasi ya zamani na kulazimika kulisafisha ili kufanya uwekezaji huo.

“Miaka ya nyuma Mkoa wa Singida tatizo la kipindupindu lilikuwa kila mara na sababu kubwa ilikuwa ni lile dampo, mimi nikaliomba eneo lile ambalo lilikuwa dampo tukakubaliana tukafikia makubaliano lakini kuondolewa taka zilizokuwepo ilikuwa inahitajika Sh.milioni sita kwa wakati huo siyo fedha ndogo.

“Sh. milioni sita Manispaa wao walidai kuwa hawana bajeti ikabidi mimi ndiye nigharamie, ikabidi nifanyie hivyo kwa makubalino kuwa watanirejeshea, nikatoa uchafu ule kama tani 1,500 na kuanza maandalizi ya ujenzi na toka wakati huo kipindupindu kikaisha Singida”alisema.

Alisema baada ya kumaliza kuondoa uchafu katika dampo hilo Manispaa walishindwa kumlipa fedha alizotumia, hivyo wakalazimika kummilikisha sehemu ya eneo hilo ambalo alijenga majengo ya biashara ikiwemo choo na bafu ya kulipia.

Alisema eneo hilo pamoja na kujenga choo na bafu cha kulipia aliwekeza pia majengo ya biashara manne ambayo yaligharimu Sh.milioni 700 na kuanza kufanya biashara. “Siku moja nipo kwenye kikao nikapata simu ya vijana wangu wakiniambiai kuwa hapa ofisini kuna watu tisa wamekuja na bunduki wanakutafuta nikahoji wananitafuta na bunduki? nikashtuka sana kwa kosa gani la kunitafuta na buduki mimi.

“Nikatoka kwenye kikao nikaenda nikakuta kweli watu hao wakiwa kwenye gari aina ya pick up wakiwa na bunduki wakasema wameniletea notisi wakidai kuwa wanataka kuvunja majengo yangu na wakinishinikiza kusaini, nikasema siwezi hadi niwasilianae na mwanasheria wangu,”alisema

Aidha, alisema kutokana na hali hiyo alilazimika kufungua kesi Mahakama Kuu ambayo ilidumu kwa zaidi ya miaka mitano, akitumia zaidi ya Sh. milioni 30 kuendesha shauri hilo.

“Nimekwenda na kesi hiyo kwa zaidi ya miaka mitano na kutumia zaidi ya Sh. milioni 30 lakini badaye wakanifuata baadhi ya watumishi wa Manispaa na madiwani wakidai kuwa nifute kesi ile ili tuzungumze nje ya Mahakama nikawakubalia”alisema

Alisema pamoja na kukubali lakini amekuwa akipata vitisho na usumbufu wa mara kwa mara kutoka kwa viongozi wa Manispaa na mkoa huo ikiwani ni pamoja na kumlazimisha kusaini mkataba mpya ambao unamuondolea haki ya umiliki wa eneo hilo.

Alisema kufuatia hali hiyo alimpigia simu Mkuu wa Mkoa wa Singida na kumtumia picha za uharibifu huo na kwenda kumuona ofisini kwake lakini hakuna alichoambulia.

“Baada ya kumpigia simu aliniambia niende ofisini lakini cha ajabu kumbe tayari alishapewa maneo na mkurugenzi hata mimi nilipojieleza hakunisikiliza na kuniambia kuwa wewe unapesa sisi tuna mamlaka na ukiendelea kuongea naweza kutuma watu wakavunje hata muda huu.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Selukamba, alipoulizwa kuhusu malalamiko hayo kwa njia ya simu alisema kuwa mkataba baina ya Manispaa ya Singida na mwekezaji huyo unamtaka kutofanya jambo lolote hadi apatiwe kibali.

Selukamba alisema eneo hilo ni ubia baina ya Manispaa na mwekezaji, hivyo hawezi kufanya kitu bila manispaa kujua, kwamba mkataba wake unamalizika mwaka 2025.

Alisema kinachofanywa na mkoa ni kwa mujibu wa mkataba ambao walikubaliana pande zote mbili, lakini mwekezaji anaonekana hataki kuufuata na kufanya kinyume na makubaliano yao.



Meneja wa Shirika la World Vision Tanzania, Kanda ya Kati, Pudensiana Rwezaula (wa pili kulia), akikabidhi vyakula vyenye thamani ya Sh. milioni 89.9 kwa Ofisa Tarafa ya Solya, wilayani Manyoni, Lydia Ntitu kwa ajili ya shule za msingi nane zilizopo wilayani humo, mkoani Singida jana. **PICHA: RENATHA MSUNGU.**

# Waandamana kupinga mapenzi ya jinsia moja

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WAUMINI wa dini ya Kiislamu mkoani Singida wamefanya maandamano ya amani ya kupinga vitendo vya mapenzi ya jinsia moja (ushoga).

Pia, wameliomba Bunge litunge sheria kali itakayotoa adhabu ya kifo kwa watu wanaojihusisha na vitendo hivyo.

Waumini hao walifanya maandamano hayo juzi, yaliyoandaliwa na Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) Mkoa wa Singida na kuongozwa na Shekhe wa Mkoa wa Singida, Issa Nassoro.

Maandamano hayo yalianzia katika Msikiti wa Taqwa na kupita Barabara ya TRA, Barabara ya Arusha, Soko Kuu, CCM makao makuu, hadi kituo cha zamani cha mabasi ambako yalipokelewa Mkuu wa Wilaya ya Iramba, Suleiman Mwenda kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba.

Waandamanaji hao walikuwa wakipaza sauti mitaani wakisema ‘Singida bila ushoga inawezekana’ huku wakiwa wamebeba mabango yenye ujumbe mbalimbali.

Baadhi ya mabango hayo yalikuwa na ujumbe uliosomeka kwamba, mashoga wote wanyongwe, heri ya ukimwi kuliko ushoga, serikali izichukulie hatua kali taasisi zinazoeneza ushoga, tunalaani vikali mapenzi ya jinsia moja (ushoga), ukahaba na ukatili wa kijinsia, tunapinga ulawiti, usagaji na ndoa za jinsia moja.

Baada ya maandamano hayo kufika katika eneo la stendi ya zamani, viongozi wa makundi mbalimbali ya taasisi za dini ya kiislamu walianza kutoa matamko ya kupinga vitendo hivyo ambavyo walidai vinakwenda kinyume na utamaduni wa Tanzania.

Juma Mdida akitoa tamko kwa niaba ya wazee wa dini hiyo, alisema mambo ya ushoga hayakubariki na hata vitabu vya dini vinayakataza na kutoa mfano wa maangamizi ya Rutu ambapo Mwenyezi Mungu alichukizwa na vitendo vichafu vilivyokuwa vikifanyika.

Mdida alisema ili kukomesha vitendo vichafu aliomba Bunge litunge sheria kwa mtu yeyote atakayebainika kujihusisha na ushoga auwawe.

Shekhe wa Mkoa wa Singida, Nassoro alisema wanamuunga mkono Dk. Harrison Mwakyembe na kutaka serikali izitaje hadharani taasisi zote zinazohamasisha ushoga.

Aidha, Shekhe Nassoro alisisitiza suala la kuiomba serikali kufanya operesheni maalumu ya kubaini nyumba za wageni ambazo zimekuwa zikihusika na masuala ya ushoga kwani zinafahamika ili hatua zichukuliwe.

Mkuu wa Wilaya ya Iramba, Mwenda alisema serikali inaunga mkono jitihada zinazofanywa na taasisi za dini kupinga vitendo hivyo.



**HABARI MBEYA**

# CHADEMA yataja dawa kukomesha ubadhirifu wa halmashauri

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimeshauri wakurugenzi wa halmashauri nchini waajiriwe na halmashauri husika kwa lengo la kuongeza uwajibikaji na kuepusha ubadhirifu wa fedha za umma.

Ushauri huo umekuja ikiwa ni siku chache baada ya Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuibua ubadhirifu wa wa fedha za umma kwenye miradi mbalimbali inayotekelezwa kwenye ngazi ya serikali za mitaa.

Katibu wa CHADEMA Kanda ya Nyasa, Gwamaka Mbughi alitoa ushauri huo mwishoni mwa wiki wakati viongozi wa kanda hiyo walipozungumza na wandishi wa habari kuhusu uchambuzi wa ripoti ya CAG kwenye halmashauri zote za kanda hiyo.

Alisema kwa mujibu wa sheria za nchi, wakurugenzi wanatakiwa wawajibike kwa halmashauri lakini kiuhalisia wanawajibika kwa Rais ambaye ndiye anawateua na hivyo kuwanyima madiwani nafasi ya kuwawajibisha pale wanapofanya makosa.

Alisema ripoti ya CAG inaonyesha baadhi ya halmashauri zilizoko kwenye kanda hiyo hazi zilifanya makosa ambayo yangeweza kudhibitiwa na wakurugenzi lakini hawakufanya hivyo na madiwani hawawezi kuwashughulikia.

"Kwa sasa madiwani hawana nguvu ya kisheria ya kumuwajibisha mkurugenzi, kuna baadhi ya halmashauri zilifanya manunuzi ambayo hayakuidhinishwa na madiwani na zipo zingine zilizofanya makosa kwenye ukusanyaji wa mapato kwa kutumia mashine za POS," alisema Mbughi.

Alisema katika baadhi ya halmashauri mashine hizo za kukusanyia ushuru zilizimwa kati ya siku tano mpaka 65 jambo ambalo lilisababisha upotevu wa mapato ya serikali kwa watumishi wa serikali kujinufaisha nayo. Alisema mkurugenzi akiajiriwa na halmashauri atakuwa anawajibika moja kwa moja kwa madiwani na hivyo watakuwa na nguvu za kisharia za kumuwajibisha pale atakapofanya makosa yanayostahili kuwajibishwa.

Aliyekuwa Mbunge wa Tunduma, Frank Mwakajoka alisema utekelezaji wa miradi unaoendelea kwa sasa katika maeneo mbalimbali unaonyesha kuwa ripoti ya CAG ijayo itaibua madudu mengi zaidi kuliko yam waka huu.

Alisema miradi mingi inatekelezwa chini ya kiwango kutokana na usimamizi duni wa viongozi wa serikali hali ambayo alisema haiwezi kudumu na inaweza ikasababisha madhara kwa watumiaji wa miradi hiyo.

Aliitaka serikali kuchukua hatua za mapema kudhibiti ubarilifu unaofanyika kwenye miradi ya serikali ili kuepusha upotevu zaidi wa fedha za umma.

"Sisi tunaishi kwenye jamii na tunashuhudia utekelezaji wa miradi ya maendeleo, sasa kwa jinsi tunavyoona tunaamini kwamba ripoti ya mwakani itakuwa mbaya zaidi, kama rais alionyesha kuchukizwa wakati anapokea ile ripoti basi ijayo atatumia na 'viboko'," alisema Mwakajoka.

Alisema dawa ya kuondoa ubadhilifu ni Katiba mpya ambayo itabadili mifumo ya uteuzi wa watendaji wa serikali hasa kwenye halmashauri na mashirika ya umma.

# Wananchi wafunguka faida ujenzi barabara njia nne

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI jijini Mbeya wamesema ujenzi wa barabara ya njia nne katikati ya Jiji hilo utasaidia kuongeza fursa za kiuchumi pamoja na kuondoa msongamano wa magari ambao umekuwa ukichelewesha baadhi ya shughuli.

Waliyasema hayo jana walipozungumza na Nipashe kuhusu utekelezaji wa mradi huo ambao unatarajiwa kuanza mwishoni mwa mwezi huu ambapo walisema utasaidia pia kupunguza ajali ambazo zimekuwa zikitokea mara kwa mara.

Mmoja wa wananchi hao, John Mwakabungu alisema kwa muda mrefu kumekuwa na msongamano wa magari katikati ya Jiji na kusababisha baadhi ya shughuli kuchelewa kutekelezwa.

Alisema kumekuwa kukiwa na msongamano mkubwa asubuhi na jioni kutokana na mwingiliano kati ya magari makubwa na madogo pamoja na barabara kuwa nyembamba.

Rehema Joseph alisema wamepata maelezo kuwa barabara hiyo itakuwa na vivuko vya juu vya watembea kwa miguu na hivyo wanaamini kuwa ajali za watu kugongwa na magari zitapungua.

"Tunamshukuru Rais Samia kwa mradi huu na tunaamini utakamilika kwa wakati na tutaanza kunufaika mapema, tumekuwa tukihangaika kwa muda mrefu," alisema Rehema.

Aliiomba serikali ikikamilisha mradi huo ianze mapema utekelezaji wa mradi wa njia ya mchepuko kwa ajili ya malori ili kupunguza matukio ya ajali.



Balozi wa India nchini Binaya Srikanta Pradhan (kulia), akijadiliana na baadhi wa wafanyabiashara walioshiriki kikao cha kujadili fursa mbalimbali za kibiashara kilichoandaliwa na Chemba ya Biashara, Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA) Mkoa wa Mbeya, juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA.**

# India yawatangazia neema wakulima maparachichi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAKULIMA wa maparachichi nchini wamepata soko la uhakika la zao hilo nchini India baada ya nchi hiyo kuitaka Tanzania kuingiza kwa wingi ikilinganishwa na nchi nyingine za kiafrika zinazozalisha.

Balozi wa India nchini Tanzania, Binaya Srikanta Pradhan juzi alisema wamefungua fursa hiyo kwa Tanzania pekee na kwamba wapo tayari kupokea parachichi nyingi kwa sababu mahitaji ni makubwa.

Akizungumza kwenye kikao cha pamoja cha wadau wa kilimo na biashara ambacho kiliandaliwa na Chemba ya Biashara Viwanda na Kilimo (TCCIA), Mkoa wa Mbeya, alisema Serikali ya India imeongeza wigo wa kupeleka parachichi kutoka Tanzania.

Balozi Binaya aliwataka wakulima kuzalisha kwa wingi parachichi zitakazokidhi ubora, kuwa na soko la uhakika nchini India na kwamba tayari wameweka mazingira mazuri ya kupokea bidhaa hizo.

Aliongeza kuwa India ipo tayari kuisaidia Tanzania kuboresha sekta ya afya ambapo watametoa ofa kwa wanafunzi wanaosomea masomo hayo kupata ufadhili wa masomo pamoja na ujenzi wa vituo vya afya na zahanati ili kuboresha huduma za matibabu.

Mwenyekiti wa TCCIA Mkoa wa Mbeya, Eric Sichinga alisema wajasiriamali wanapaswa kuchangamkia fursa hiyo kwa kuzalisha mazao ya kimkakati ikiwemo parachichi, mpunga na maharage.

Alisema TCCIA itaendelea kuwatafutia fursa na masoko wazalishaji wa mazao, huku akiwahimiza kuzingatia ubora na kuongeza thamani ya mazao yao ili kujipatia kipato.

Mku wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa alisema jukumu la serikali ni kuhakikisha wananchi wananufaika na fursa za kiuchumi zinazojitokeza.

Alisema miongoni mwa hatua zinafanyika ni kutafuta masoko ili wakulima kuuza maeneo mbalimbali duniani na kuongeza kuwa Mkoa wa Mbeya ni eneo ambalo limebarikiwa kuwa na uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara ukilinganisha na mikoa mingine, hivyo watachangamkia fursa hiyo.

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) Idara ya Kilimo Biashara, Dk. Ibrahim Kadigi aliuomba Ubalozi wa India kuchagua wanachuo waliofanya vizuri kwenye masomo hayo kwenda kujifunza masuala ya kilimo nchini India.

Alisema kwa kufanya hivyo itasaidia kuzalisha vijana wabobezi kwenye masuala ya kilimo kwani watajifunza teknolojia za kisasa kuhusu kilimo na kuisaidia Tanzania.

Baadhi ya washiriki akiwamo, Elizabeth Mwakatobe ambaye ni mfanyabiashara alisema wapo tayari kutumia fursa ya kuuza bidhaa zao nchini India.

## Makamu wa Rais awakumbusha wajibu watumishi wa umma

**Na Mwandishi Wetu**

Makamu wa Kwanza wa Rais Othman Masoud Othman, amesema kufuata maadili na sheria za kazi kwa watumishi wa umma ni jambo muhimu katika maendeleo ya nchi.

Aliyasema hayo juzi wakati akifungua mafunzo ya watumishi wa taasisi zilizo chini ya ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kuhusu maadili ya kazi na usalama kazini.

Othman alisema utumishi wa umma Zanzibar umeanza miaka kadhaa iliyopita kwa kupitia katika hatua mbalimbali na kwamba iwapo nchi inataka kujenga utumishi bora ni vyema pia kuangalia na historia.

Alisema Zanzibar wana kila sababu ya kuutunza na kuufanya utumishi wa umma utukuke kutokana na historia yake iliyoanzia mwaka 1890.

Alisema kwamba mfumo rasmi ulioweka mawaziri ulikuja mwaka 1960 na kukatolewa muongozo na sheria za jumla za utumishi ulioweka
wajibu kwa viongozi mbali mbali wakiwemo watumishi , viongozi mawaziri na wakurugenzi sambamba na kuwepo kwa Kamisheni ya Utumishi wa Umma inayosimamie utumishi wa kiserikali.

Aidha aliwataka watumishi wa umma kufanya kazi kwa kuzingatia wujibu, taratibu na kanuni za kiutumishi ambazo unakwenda na mfumo wa kikatiba katika kuchangia maendeleo ya nchi kwa haraka.

Pia, aliwataka watumishi na viongozi kuhakikisha wanafuata maadili kutokana na umuhimu wake hasa katika utoaji wa huduma kwa uaminifu mkubwa wa kimaadili.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Harous Said Suleiman, alisema mafunzo hayo ni katika fursa muhimu kwa watendaji na wafanyakazi katika utoaji wa huduma na kujenga ufanisi.

Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Dk. Omar Dadi Shajak, alisema mafunzo hayo yanalenga kutekeleza kwa vitendo agizo la serikali la kuhakikisha kwamba watumishi wote wa umma wanapatiwa taaluma juu ya sheria, maadilini na usalama kazini.

# Waziri avutiwa na ushirikiano wasemaji vyama vya siasa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera na Uratibu wa Shughuli za Baraza la Wawakilishi, Hamza Hassan Juma amesema ni jambo la faraja kuona wasemaji wakuu wa vyama vya siasa wanakaa pamoja na kushirikiana katika shughuli za kuwaunganisha Wazanzibari.

Aliyasema hayo juzi katika hafla maalum ya chakula cha futari kilichoandaliwa na Umoja wa Klabu ya Waandishi wa Habari Zanzibar (ZPC) ambapo iliwakutanisha wadau mbalimbali wakiwemo viongozi wa vyama vya siasa.

"Ninapowaona wasemaji wakuu wa vyama vikubwa vya siasa hapa Zanzibar, wanakaa meza moja, wanakula pamoja, wanasalimiana, wanakumbatiana kwa kweli mimi kazi yangu inakua ni nyepesi, siku ambayo watakayoamua kwamba fulani haendi na mie siendi kwa kweli pale ofisini nitakua sina raha," alisema.

Alisema kazi waliyoifanya viongozi hao wa vyama vya siasa ya kuwaunganisha Wazanzibari kuwa kitu kimoja kuacha tofauti zao wanampa faraja Rais wa Zanzibar, Dk Hussein Ali Mwinyi.

Hamza alisema viongozi wakuu wanafarajika kuona ushirikiano huo wa kuhakikisha amani na utulivu unapatikana nchini na wananchi wanaendelea na shughuli zao.

Alisema bila ya waandishi wa habari kazi wanazofanya viongozi wa serikali na wa vyama vya siasa ingekua ngumu lakini waandishi wa habari wanafanya kazi kubwa ya kuhakikisha na kutangaza shughuli za kiserikali, kimaendeleo na kijamii.

Aidha, alisema kazi ya uwandishi wa habari ni ya uweledi na ni kazi ambayo inahitaji maarifa na wanakazi kubwa ya kutoa habari sahihi na hakuna chombo cha habari kilichokwenda kinyume na maadili na miiko ya uandishi wa habari.

Aliwataka waandishi wa habari wasione tabu kuzisema changamoto zilizopo ili serikali kuzifanyia kazi na ikiwa wanasifu bila ya kueleza changamoto itashindwa kuzifanyia kazi.

Hamza alisema serikali inafarijika kuona vyombo vya habari vinafanya kazi vizuri, hivyo ni vyema waandishi wa habari kuendelea kuisaidia nchi katika kutoa taarifa sahihi.

Akizungumza katika hafla hiyo, Katibu wa Idara ya Itikadi, Uenezi na Habari CCM Zanzibar, Mbeto Khamis Mbeto alisema, waandishi wa habari wanafanya wajibu wao vizuri, wanaripoti matukio muhimu ya serikali.

Mbeto alisema Zanzibar yenye maendeleo na utulivu ni lazima kuwa na Zanzibar ya maridhiano na ndiyo suluhisho la Wazanzibari na siyo kitu chekingine.

Alisema CCM inaichukulia upinzani siyo uadui bali ni kioo cha kujitathmini ili kuwatumikia kwa ubora Wazanzibari na wapinzani wanamchango mkubwa katika kuongoza nchi.

Mkurugenzi wa Idara ya Habari na Mawasiliano ya Umma kutoka Chama cha ACT Wazalendo, Salum Bimani, alisema nchi ni ya wananchi wote na inahaki kwa kila mzanzibari, hivyo ni vyema serikali kusimamia yale yote mazuri waliyokubaliana.

Bimani alisema miongoni mwa mambo yaliokubalika katika kikosi kazi hicho ni kupata tume huru ya uchaguzi, daftari safi la wapiga kura na masuala yote ya uhuru na haki katika nchi ili amani na utulivu izidi kuendelea.

Mwenyekiti wa ZPC, Abdalalh Abrahman Mfaume, alisema lengo la hafla hiyo ni kuwakutanisha wadau wa habari ikiwemo wanasiasa ili kuzungumza mambo mbalimbali kwa mustakbali wa kuendeleza umoja na maridhiano na amani ya nchi.




Mkurugenzi wa Kampuni ya ununuzi wa Tumbaku ya Mkwawa Leaf, Mattew Kapnias (katikati) na Msaidizi wake, Richard Sinamtwa (kulia), wakikabidhi msaada wa bidhaa na vyakula vya futari kwa Mkuu wa Gereza la Mahabusu la Mkoa wa Tabora, SSP Ali Lupululu, gerezani hapo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakala ukaguzi wa bidhaa, chakula watakiwa kufika vijijini

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAKALA wa Ukaguzi wa Bidhaa za Chakula na Vipodozi Zanzibar wametakiwa kufanya ukaguzi hadi vijijini ili kuepuka matukio ya wananchi kutumia vyakula ambavyo vimepitwa na muda wa matumizi ili kuepusha athari za kiafya.

Rai hiyo ilitolewa jana na Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi, Mohamed Ahmada Salum wakati wajumbe wa kamati hiyo walipotembelea ofisi ya wakala wa ukaguzi wa bidhaa za chakula na vipodozi mjini Unguja.

Alisema ukaguzi wa bidhaa za chakula na vipodozi ni muhimu ambao lengo lake kuona wananchi wanatumia vyakula na bidhaa nyingine zikiwa salama kwa ajili ya afya zao.

"Bodi ya wakala wa ukaguzi wa bidhaa za chakula na vipodozi nendeni vijijini mkafanye ukaguzi zaidi wa bidhaa za vyakula ambapo baadhi ya wafanyabiashara hupeleka bidhaa zilizopitwa na muda wa matumizi maeneo hayo kitendo ambacho kinatishia hali za afya zao"alisema.

Naibu Waziri wa Afya, Hassan Khamis Hafidh, alisema wamejipanga kuhakikisha masuala ya ukaguzi wa bidhaa za vyakula yanapewa kipaumbele ili afya za wananchi kuwa salama.

Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Wakala wa Ukaguzi wa Bidhaa za Chakula na Vipodozi, Dk. Burhani Othman Said, alisema wameimarisha majukumu ya utendaji wa kazi zao ikiwemo kuimarisha maabara ya ukaguzi wa bidhaa za vyakula kwa kiwango cha kimataifa.

Alisema ukaguzi wa bidhaa ndiyo kipaumbele cha taasisi hiyo ambapo wanapambana na changamoto mbalimbali ikiwemo ujanja wa wafanyabiashara katika kuingiza bidhaa za vyakula ambavyo vimepitwa na wakati.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO......07......OF 2023**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE RAPHAEL NGODA MKUNDAWANTU**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LATER OF ADMINISTRATION**
**BY EDITH MKANDE**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above name deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration id made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 11 day of May 2023
Dated at Korogwe this 11 day of April 2023

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA CHATO**
**MAHALI LILIPO CHATO**
**MAOMBI/RUFAA NA. 27 MWAKA 2022**
**HELENA BENEDICTO BAKENGELEHI.....MWOMBAJI/MRUFANI**
**DHIDI YA**

(1) Fikiri Manambali
(2) Amos Ngale
(3) Leonard Godfrey
(4) Tabita Samweli Mwinula
(5) Amos Ngaye
(6) Mussa
(7) Nyanjige Jejeje
(8) Georgina Hamis Kapi.

**MJIBU MAOMBI/MRUFANIWA**

**Kwa...Fikiri Manambali na wenzake 7**
Fahamu kwamba shauri hili limepangwa kuitwa/kusikilizwa tarehe 19 mwezi wa 4 mwaka 2023 saa 2:30 asubuhi mbele ya MH. A.M. KAPINGA Mwenyekiti wa Baraza.

Hivyo unaarifiwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa pamoja na utetezi/majibu yako ndani ya siku 21.

AMRI hii imetolewa leo kwa mkono wangu na Lakiri/Mhuri wa Baraza hii leo tarehe 28 Mwezi wa 05 Mwaka 2023.

....Mwaka 2023.....
MWENYEKITI

---

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA DODOMA**
**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**SHAURI LA MIRATHI NA.10 YA 2022**
Maombi ya barua za usimamizi wa Mirathi ya
**MARY BUSI BAHATI.............MAREHEMU**
**NA**
- **ERNESTILLA JOHN BAHATI**
- **STANSLAUS LUBUVA BAHATI...WAOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(kanuni ya 75 na 76)**
Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hilo katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua ya usimamizi wa mirathi kwa waombaji waliotajwa hapo juu.
Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 02 mwezi mei mwaka 2023
Imetolewa leo tarehe 27 mwezi wa Machi, 2023

NAIBU MSAJILI
MAHAKAM KUU YA TANZANIA
DODOMA

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**SELLA SAUSI BENSON** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.2549/0043 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia ALPHA HIGH SCHOOL mwaka 2016. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **POLISI TAARIFA: DAR/CHU/RB/115485/2023**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Njombe**
**Kituo cha Njombe Mjini**
**Mkoa wa Njombe**
**Usimamizi wa mirathi Na. 32/2023**
**MTAVIKODI DAGAVATWA MLIGO......Marehemu**
**IBRAHIMU MTAVIKODI MLIGO......Msimamizi**
**TAARIFA KWA WADAI**
(Kanuni ya 9 (1) ya Nyongeza ya V ya Sheria ya Mahakimu wa Mahakama Sura ya 11 Rejeo la 2019)

**TAARIFA** inatolewa hapa kwa wote wanaodai kuwa na madai yanayohusiana na mali za marehemu, mtajwa hapo juu **MTAVIKODI DAGAVATWA MLIGO**, aliyefia Njombe tarehe 02 Mei, 1942, na Mahakama kunipa barua ya usimamizi wa mirathi hiyo **IBRAHIMU MTAVIKODI MLIGO** siku ya tarehe **14 April 2023,** hapa sasa wanatakiwa kunipa madai yao kwangu kupitia namba sanduku langu la barua..............Njombe au namba ya simu **0765040641**, au kuniletea kwa binafsi, ndani ya siku 14 kuanzia tarehe ya kutangazwa taarifa hii ambapo muda wake utapoishia nitaendelea kukabidhi mali za marehemu kwa warithi wanaostahili, nikizingatia tu madai ambayo nitakuwa nimearifiwa.

IBRAHIMU MTAVIKODI MLIGO

Imepitishwa

---

## KUPOTEA KWA PASPORT



**HALELUYA IMANUELI MOSHI** Mtajwa hapo juu amepotelewa na passport yenye NO, TAE 035054 iliyotolewa na ofisi ya uhamiaji tarehe 6 Mwezi July mwaka 2018. Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi
**KIL/MOS/RB/119887/2023**

---

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**IN THE DISTRICT REGISTRY OF ARUSHA**
**AT ARUSHA**
**LAND APPEAL NO. 66 OF 2022**
**DAUDI LOSIYO@ DAUDI LOSIYO KIVYO ...............APPELANT**
**VERSUS**
**MWANGAO SADIKI & 5 OTHERS...................RESPONDENTS**
**NOTICE OF MENTION**
**TO:**
- **NELSON LOTA**
- **CHARLES TEMBA**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for mention in the high court at Arusha on the 22nd day of May 2023 at 9:00am o'clock in the forenoon, before **HON.B.K.PHILLIP, JUDGE.**
You may appear in person or by advocate or agent duly authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all documents upon which you intend to relay in support of your case.
**TAKE FURTHER NOTICE THAT** in default of your appearance on that day and time before mention the court may proceed in your absence
**GIVEN** under my **HAND** and **SEAL OF THE COURT** this 29th day of March 2023

.......................................................................
**DEPUTY REGISTRAR**
**ARUSHA**

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**TULANYILIKA NAFTARY TWEVE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0217/0050/2013** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **PERAMIHO GIRLS SECONDARY SCHOOL** mwaka 2013. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **ARU/ARU/RB/119053/2023**

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**PETRO MSABI WEREMA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.4993-0122 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia RODAN SECONDARY SCHOOL mwaka 2014. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi .
**POLISI TAARIFA: LIN/LIN/RB/132945/2023**

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**JULIUS KAZEMBELA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index number **S0757-0051** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **KYELA SEKONDARI** mwaka 1999. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Control namba: **11826942.**

---

## KUPOTEA KWA KADI ZA BAJAJI

**KALOS COSMA KAVISHE** anatangaza kupotelewa na kadi ya bajaji yenye namba za usajili **MC 192 BAZ,** kadi ya bajaji yenye namba za usajili **MC 155 BPZ.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha Polisi.
Taarifa ya Polisi: **DAR/URA/RB /52877/2023.**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**KALOS COSMA KAVISHE** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 993 CFV.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi.
Taarifa ya Polisi: **DAR/URA/RB /52877/2023.**

---

## KUPOTEA KWA KADI ZA BAJAJI

**KALOS COSMA KAVISHE** anatangaza kupotelewa na kadi ya bajaji yenye namba za usajili **MC 832 BWJ,** kadi ya bajaji yenye namba za usajili **MC 715 BRN.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha Polisi.
Taarifa ya Polisi: **DAR/URA/RB /52877/2023.**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ALEXANDER GABRIEL MARGWE** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 908 CSP,** Chasis namba **LZL15P904LHK53808,** Engine namba **KL162FMJ201053808.** Kwa yeyote atayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
TAARIFA YA POLISI: **MAN/BAB/RB/130785/2023**

---

## TANGAZO LA KUPOTEA KWA HATI YA KIWANJA

**MAURICE GABRIEL ONYANGO** anatangaza kupotelewa na hati ya kiwanja Namba **274 Block 'D'** chenye jina la **GABRIEL ONYANGO** kilichopo High Density Karume. Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Control namba: **9910836405534.**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ANTHONY LUYIRIKA KAFUMBE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya HONDA yenye usajili namba **T 681 APR,** CHASSIS NAMBA: **RD11027809** na ENGINE NAMBA: **B20B1027855.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: **ARU/ARU/RB/134248/2023**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

SHAWEJI MOHAMED TIMBULO anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TRAILER yenye usajili namba T.144 APN . kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: MKB/RB/69/2022

---


**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 0677020701**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**Website: www.ippmedia.com**



**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA




Anga la mji mkuu wa Sudan wa Khartoum limeendelea kutanda wingu la moshi unaotokana na milipuko ya mabomu. **PICHA: AFP**

# Khartoum yazidi kuteketea

- Mabomu angani, ardhini

**KHARTOUM,** Sudan

MJI mkuu wa Sudan, Khartoum, unazidi kukabiliwa na mapigano makali kwa siku ya tatu mfululizo na kusababisha vifo vya watu 100, na kuteketeza mali mbalimbali.

Mapigano makali yaliibuka Jumamosi iliyopita baada ya kutokea mzozo wa kimadaraka kati ya Kamanda wa Jeshi, Jenerali Abdel-Fattah al-Burhan, na Jenerali Mohammed Hamdan Dagalo, ambaye ni Mkuu Kikundi Maalum cha kijeshi (RSF).

Sasa mashambulizi yanafanyika kutoka angani na imeshuhudiwa yakiendelea kurushwa katika maeneo mbalimbali ya mji mkuu Khartoum na mji jirani wa Omdurman.

Milio ya risasi na mabomu ilisikika karibu na makao makuu ya jeshi, huku moshi mweupe ukionekana kutoka eneo hilo.

Wakazi wa jiji la Khartoum, walisalia kwenye nyumba zao huku wakiripoti kukatika kwa umeme na matukio kadhaa ya uporaji.

Majenerali hao wawili ni washirika wa zamani ambao walipanga kwa pamoja mapinduzi ya kijeshi ya Oktoba mwaka 2021, ambayo yaliharibu mchakato wa mpito na wa muda mfupi wa kuelekea kwenye demokrasia.

Hata hivyo, wababe hao wamekaidi kusitisha mapigano na kusema hawatofikia makubaliano yoyote, huku kila upande ukimtaka mwingine kujisalimisha.

Hata hivyo pande zote mbili zina wafadhili wa kigeni wenye nguvu, jambo linaloweza kupelekea uwezekano mkubwa wa kusababisha shinikizo la kidiplomasia.

Tangu mapigano yalipozuka siku ya Jumamosi, raia wapatao 97 wameuawa na mamia ya wengine wamejeruhiwa, hayo ni kwa mujibu wa Shirika la Madaktari la Sudan, linalounga mkono vuguvugu la kidemokrasia.

Hata hivyo, hakujakuwa na taarifa rasmi kuhusu idadi ya wapiganaji waliouawa mpaka jana.

Mapigano hayo yaliyojumuisha silaha kali kama mizinga, makombora na ndege za kivita katika maeneo yenye watu wengi katika mji mkuu wa Sudan, na kusababisha hali ya kutisha ambayo haijawahi kushuhudiwa.

Sudan ina historia ndefu ya mapigano ya wenyewe kwa wenyewe, lakini mapigano mengi yamekuwa yakifanyika katika maeneo ya kikabila na yaliyo mbali na mji wa Khartoum.

### MATAIFA YAPATA HOFU

Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken amesema wasiwasi umetanda kutokana na kile kinachoendelea Sudan,

"Kuna wasiwasi mkubwa kwa sote kuhusu mapigano na ghasia zinazoendelea nchini Sudan. Tishio ambalo linawakabili raia na ambalo linalikabili taifa la Sudan. Tishio hilo linaweza kusambaa katika eneo zima." alisema

Mwakilishi Maalum wa Umoja wa Mataifa nchini Sudan Volker Perthes, amezidi kusikitishwa na hatua ya vikosi pinzani vya kijeshi kutoheshimu kikamilifu usitishaji mapigano wa muda uliokubaliwa na pande zote hapo jana ili kuwahamisha majeruhi.

### AFRIKA YAJITUTUMUA

NCHI za Afrika zimeonekana kukerwa na mapigano hayo kiasi viongozi mbalimbali wametoa maoni yao kukemea hali hiyo ambayo wameiita inatia aibu bara hilo.

Kumekuwa na msururu wa maoni na wito wa kusitishwa kwa mapigano nchini humo.

Afrika Kusini ilitaja hali inayoendelea Sudan kuwa ya kusumbua na kutoa wito kwa pande zinazopigana kuweka chini silaha kuwaepushia watu na mahangaiko wakati wa mwezi mtukufu wa Ramadhani.

Rais wa Uganda Yoweri Museveni, alisema ni muhimu zaidi kusitisha uhasama katika kukomesha maafa na kejeli kwa Afrika.

Kwa upande wa Rais wa Kenya, William Ruto aliwataka viongozi wa kanda kuchukua msimamo thabiti kurejesha amani katika mji wa Khartoum.

Mamlaka ya Kenya ilisema inapanga kuwahamisha raia wake 3,000 waliokwama nchini humo.

Waziri Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed, alisema mapigano hayo yanakinzana na kanuni na maadili ya Sudan ya muda mrefu na yenye mizizi mirefu.

Baraza tawala la kijeshi nchini Chad, limeamuru kufunga mpaka wake na Sudan na kuwataka wanaopigana waanze mazungumzo.

Rais wa GuineaBissau,Umaro Sissoco Embalo - ambaye pia ni mwenyekiti wa Jumuiya ya Kiuchumi ya Afrika Magharibi (Ecowas), ametaka kuwepo kwa utulivu na mazungumzo.

### MKUU RSF AJITETEA

Maoni mapya kutoka kwa mmoja wa wababe wawili wanaohusika katika mzozo mkali. Jenerali Mohammed Hamdan Dagalo, maarufu kama Hemeti, yanaonyesha kutoa wito kwa jumuiya ya kimataifa kuingilia kati.

Katika jumbe za Twitter zilizotumwa asubuhi ya jana anatoa wito wa kuchukuliwa hatua dhidi ya uhalifu wa mpinzani wake, kiongozi wa jeshi Jenerali Abdel Fattah al-Burhan.

Anadai kuwa wanajeshi wake wanapigana dhidi ya Waislamu wenye itikadi kali. Mkuu huyo wa RSF alisema vita anavyoendesha ni gharama ya demokrasia.

Alisema askari wake hawakushambulia mtu yeyote na wanajibu tu kuzingirwa na kushambuliwa kutoka kwa wanajeshi wa serikali.

"Tunapigania watu wa Sudan kuhakikisha maendeleo ya kidemokrasia, ambayo wamekuwa wakiyatamani kwa muda mrefu."

### RAIA HAWANA CHAKULA

Wakazi wa mji mkuu wa Khartoum, wanakabiliwa na ukosefu wa chakula na maji baada ya siku tatu za mapigano makali.

Mwanaharakati wa haki za binadamu Duaa Tariq, ameiambia BBC, kuwa wanapanga upinzani wa amani dhidi ya utawala wa kijeshi kutokana na ghasia hizo na kutoa wito wa kuwepo kwa mabadiliko ya amani kwa serikali ya kiraia nchini humo.

Alisema watu wamekosa umeme kwa siku mbili, maduka yamefungwa na wakazi wa eneo hilo hawakuwa na wakati wa kutafuta chakula katika maeneo mengi ya mji mkuu.

Tariq alisema hayo katika kipindi cha Newsday cha BBC World Service, aliongeza milio ya milipuko na risasi ilikuwa mikubwa sana asubuhi ya jana, huku mapigano yakiendelea katika miji ya karibu.

Aliongeza kuwa hali hiyo ni ya kutisha kwa familia yake, kwani dada yake na mpwa wake mdogo wamekimbia mapigano kwenda kukaa naye karibu.

HABARI MICHEZO

# BAO LA KIBU LAGEUKA GUMZO BETIKA MTOKO WA KIBINGWA

Na Mwandishi Wetu

BAO la pili la Simba lililofungwa na Kibu Denis limekuwa gumzo kwa mashabiki wa 'Betika Mtoko wa Kibingwa' walioshuhudia laivu dabi ya watani wa jadi, Simba na Yanga kwa mara ya kwanza juzi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

**Kibu aliandika bao hilo dakika ya 32 kwa shuti kali akipigilia msumari ushindi wa mabao 2-0 wa Simba mbele ya watani wao, Yanga katika mechi ya mzunguko wa pili ya Ligi Kuu Tanzania Bara, bao jingine lilifungwa na Hanock Inonga dakika ya pili ya mchezo.**

Mabao hayo yamekuwa gumzo kwa mashabiki 100 wa Betika Mtoko wa Kibingwa waliokuwa miongoni mwa maelfu walioishuhudia mubashara dabi hiyo juzi huku mashabiki wa Simba wakiwatambia wa Yanga kwamba wasipoangalia hata kibao cha ubingwa kinaweza kubadilika kwani ligi bado, hivi sasa Yanga ina pointi 68 na Simba 63, zote zikisaliwa na mechi nne mkononi.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti uwanjani hapo juzi, mashabiki wa Betika Mtoko wa Kibingwa ambao ni wanazi wa Simba, hiyo ikiwa mara yao ya kwanza kuishuhudia dabi hiyo mubashara walisema wamekoshwa na kiwango cha timu yao, wakiwakebehi Yanga kwamba kilichowaponza ni kwenda na matokeo mkononi.

Sharifu Nalinga wa Mtwara ambaye ni mnazi wa Simba alisema, bao la pili la Kibu lilimpa furaha mara dufu kwa timu yake hiyo na kuishukuru Kampuni ya Betika kwa namna walivyompa fursa ya kuitizama dabi mubashara kwa mara ya kwanza.

"Tangu tumefika Dar es Salaam ilikuwa ni furaha kwangu hadi leo (jana) naondoka, Betika imejitofautisha, tumepokelewa kistaa, tumeshiriki bata la msimu na kuwashuhudia 'laivu' watu mbalimbali maarufu ambao nilikuwa nikiwaona kwenye televisheni," alisema Nalinga.

Mnazi mwingine wa Simba, Constantine Mbele wa Ruvuma, alisema nyota njema ya ushindi huo ilianza kuonekana tangu alipowasili Dar es Salaam Jumamosi iliyopita.

"Mapokezi tuliyopewa yalinipa amani mno, tukiwa uwanjani tukapata bao la mapema, niliona kabisa Yanga tunawamudu, japo mwanzoni walikuwa wanachonga sana hadi nikaogopa, Kibu alipofunga bao la pili nikajua habari yao imeishia pale, kiukweli ninafuraha mno, nawashukuru zaidi Betika kwa kuleta Promosheni ya Mtoko wa Kibingwa, ambayo bila hii, labda nisingepata fursa ya kuishuhudia dabi laivu," alisema Mbele.

Bakari Kipopele wa Kagera ambaye ni shabiki kindakindaki wa Yanga, aliwapongeza watani zao, Simba kwa ushindi akikiri mechi ilikuwa ngumu.

Mashabiki hao wameondoka jana Dar es Salaam baada ya kuwapo tangu Ijumaa, kabla ya dabi hiyo juzi Jumapili, walishiriki kwenye bata la msimu katika hafla iliyofanyika Kidimbwi.

Ofisa Habari wa Betika Tanzania, Juvelinaus Rugambwa, alisema msimu wa tano wa Promosheni ya Mtoko wa Kibingwa umefikia tamati na wateja wao wataendelea kupata vitu vingine vizuri zaidi.

"Washindi wetu 100 kutoka maeneo mbalimbali nchini ni mabalozi kwenye promosheni hii na namna walivyopokelewa na kushiriki kwenye bata la msimu kabla ya kuishuhudia dabi laivu kwa gharama za Betika.

"Kwenye bata la msimu, kulikuwa na burudani kutoka kwa wanamuziki mbalimbali wakiongozwa na Christian Bella, wachambuzi, Mussa Husein na Ibra Kasuga kabla ya kwenda kwa Mkapa kwa king'ora kuishuhudia dabi hiyo na leo (jana) wale wa mikoani wameondoka kwa ndege, gharama zote zikiwa za Betika," alisema.




Mashabiki wa soka waliogharamiwa na Kampuni ya Betika wakifurahia mabao katika mechi ya Simba na Yanga iliyochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi. Simba ilishinda mabao 2-0. **MPIGAPICHA WETU**

# Prisons yapania kuvuna pointi 12 kujinusuru

Na Saada Akida

KOCHA Mkuu wa timu ya Tanzania Prisons, Mohammed Abdallah 'Bares', amesema mpango wake ni kukusanya pointi 12 katika michezo minne iliyosalia kabala ya Ligi Kuu Bara kufikia ukingoni mwezi ujao.

Tanzania Prisons wako nafasi ya 10 katika msimamo wa ligi hiyo wakiwa wamekusanya pointi 28, hivyo wanahitaji alama zote 12 ili kujiondoa katika nafasi ya kucheza mechi za mchujo 'Play Off' mwishoni mwa msimu ili kujinusuru kushuka daraja.

Akizungumza na gazeti hili jana, Bares alisema mechi zilizosalia mbili watakuwa ugenini dhidi ya Geita Gold FC utakaopigwa Aprili 24, mwaka huu, na tayari wako Geita kwa ajili ya mchezo huo.

Alisema mechi nyingine ya ugenini wanayohitaji alama tatu ni dhidi ya Kagera Sugar itakayopigwa Mei 14, mwaka huu na baada ya michezo hiyo watakuwa na mechi mbili nyumbani watakapowakaribisha KMC FC na Mei 28, mwaka huu na kisha dhidi ya Yanga.

"Hizi mechi ni muhimu sana kwetu kushinda kwa sababu tunahitaji kutoka katika hii nafasi na kupanda nafasi za juu kwa sababu huu muda kila timu inapambana kujinusuru kushuka na kutocheza Play Off, hali kadhalika, na sisi hatutaki kukutana na hayo mambo mawili," alisema Bares.

Alisema kwa kutambua ugumu wa michezo hiyo minne na kuhitaji alama zote 12, wanalazima kujiandaa vizuri kuhakikisha wanapata pointi sita ugenini na nyumbani ili kufikia malengo yao.

Bares alisema kuwa kwa sasa ligi imekuwa ngumu hasa kutokana na kila timu kuhitaji kutumia michezo minne iliyosalia kutafuta pointi muhimu kufikia malengo yao na kwamba wanakwenda kucheza dhidi ya Geita Gold FC wakiwa imara.

## Meridianbet sasa yaja na kitu kipya

Na Saada Akida

MKUU wa Kitengo cha Masoko na Mawasiliano Meridianbet Tanzania, Martin Nkurlu, amesema kampuni hiyo ya mchezo wa kubashiri imekuja na kitu kipya kwa mashabiki wa soka na michezo mingine kwa kuwaletea 'Sloti ya Bursting Hot 5'.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nkurlu alisema hii ni moja ya sloti rahisi kucheza na kushinda mchezo wa matunda wenye maudhui ya kizamani katika michezo mbalimbali ikiwamo soka na mingine.

Alisema kupitia msemaji itakupeleka kwenye uwanja wa Kasino ya Mtandaoni kisha utatakiwa kutafuta jina la Bursting Hot 5 ambapo utaona mchezo wenye muonekano mzuri kabisa ukiwa na matunda mbalimbali.

"Weka dau lako kisha bonyeza kitufe cha "start/anza" kuanzisha mchezo, subiri alama zizunguke na zikupe ushindi mkubwa. Kumbuka, kila dau utakaloliweka, linaweza kukupatia faida stahiki, kwenye Sloti ya Bursting Hot 5 na nyinginezo zinakupatia chaguo la kucheza 'Auto Play', ambapo utacheza moja kwa moja," alisema Nkurlu.

Alisema ushindi ndani ya Bursting Hot 5 kutoka Kasino ya Mtandaoni unakuhakikisha kushinda mpaka mara 6,000 ya dau lako endapo tu utapanga alama tano za lucky 7.

## The Ngoma Afrika ndani ya miaka 30

Na Sabato Kasika

BENDI ya muziki wa dansi ya The Ngoma Africa inayofanya shughuli za muziki nchini Ujerumani, inatarajia kufanya sherehe ya kutimiza miaka 30 tangu kuanzishwa kwake mwaka 1993.

Kiongozi wa bendi hiyo, Ebrahim Makunja 'Kamanda Ras Makunja', ambaye pia ni mwaanzilishi wake, alisema The Ngoma Africa ni miongoni mwa mabalozi wa kuutangaza muziki wa Tanzania ughaibuni.

"Bendi hii ilianzishwa Agosti 13, 1993 kwa madhumuni ya kuutangaza muziki wa dansi wa Tanzania na Afrika Mashariki kwa ujumla, tangu kuanzishwa kwake imekuwa bendi pekee ya Kiafrika iliyodumu kwa miaka mingi barani ulaya na kufanikiwa kuteka maelfu ya mashabiki wa dansi," alisema Makunja.

Makunja alisema bendi hiyo ni balozi mzuri wa Kiswahili, katika majukwaa ya kimataifa kutokana na tungo za nyimbo nyingi zinazoimbwa kwa lugha hiyo ikiwamo wimbo wa 'Mwenye kukaanga mbuyu'.

"Tunapoongelea utamaduni, sanaa za maonyesho na muziki kwa upana, ni tasinia inayoiwakilisha jamii, taifa katika tufe la dunia na hapa ndio pa kuitilia maanani tasinia hii na wasanii kwa ujumla wake," alisema.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

#### NAGELSMANN NA CHELSEA

KLABU ya Chelsea imekutana na kocha wa zamani wa Bayern, Munich, Julian Nagelsmann wakati huu wakiendelea na harakati za kumtafuta kocha wao wa kudumu baada ya kutimuliwa kwa Graham Potter. ***(Athletic)***

#### ENRIQUE ASIKITISHWA CHELSEA

KOCHA wa zamani wa Hispania, Luis Enrique, alisikitishwa kwa kuikosa nafasi ya kuwa kocha wa Chelsea kabla ya mechi ya kwanza ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Real Madrid, lakini anaonekana ni kocha anayepewa nafasi kubwa zaidi kwa sababu anaweza kusaidia kumsajili kinda wa Barcelona mwenye umri wa miaka 18, Gavi. ***(AS)***

#### HAALAND ATAKIWA MADRID

KLABU ya Real Madrid inataka kutumia mwanya wa kipengele katika mkataba wa mshambuliaji wa Manchester City, Erling Haaland mwenye umri wa miaka 22, kumsajili mshambuliaji huyo wa Norway katika msimu wa majira ya joto wa 2024. ***(Fichajes)***

#### VLAHOVIC AWANIWA ARSENAL

ARSENAL inataka kumnunua mshambuliaji wa Juventus, Dusan Vlahovic, mwenye umri wa miaka 23, huku mshambuliaji wa Everton, Dominic Calvert-Lewin, 26, akiwa chaguo lao lingine kama watashindwa kumpata Mserbia huyo. ***(Football Insider)***

#### BELLINGHAM KUBAKI

KIUNGO wa kati wa England, Jude Bellingham mwenye umri wa miaka 19, angependelea kubakia Borussia Dortmund na kutathmini tena mustakabali wake mwaka 2024 kuliko kufanya uhamisho ambao haufai kwake msimu huu wa majira ya joto. ***(Athletic)***

#### LIVERPOOL WAKO SAHIHI

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Liverpool, Robbie Fowler, anaamini 'Wekundu' hao wako sahihi kutotumia sehemu kubwa ya bajeti yao ya uhamisho kwa Jude Bellingham msimu huu wa majira ya joto kwani wanahitaji marekebisho makubwa katika sehemu yao ya kiungo. ***(Mirror)***

#### OSIMHEN AHUSISHWA UNITED

MSHAMBULIAJI wa Napoli, Victor Osimhen, amekuwa akihusishwa na Manchester United, lakini mchezaji huyo wa kimataifa wa Nigeria mwenye umri wa miaka 24, anaonekana kuwa ana furaha katika klabu hiyo ya Italia. ***(TG5 via Manchester Evening News)***

#### PEP KUWABAKISHA

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, anashinikiza kuwabakisha kiungo wa kati wa Ujerumani, Ilkay Gundogan mwenye umri wa miaka 32 na mchezaji wa Ureno Bernardo Silva, 28, katika klabu hiyo licha ya wachezaji wote wawili kuhusishwa na uhamisho msimu huu wa majira ya joto. ***(Football Insider)***

#### WEGHORST ATAKIWA BESIKTAS

KLABU ya Besiktas inataka kumsajili tena mshambuliaji wa Uholanzi, Wout Weghorst, huku Manchester United ikiwa na uwezekano wa kubadilisha uhamisho wa mkopo wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 kutoka Burnley kuwa wa kudumu. ***(Goal)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ULAYA



# ARTETA: ARSENAL SASA INA KAZI KUBWA YA KUFANYA

**LONDON,** England

MIKEL Arteta amesema Arsenal walijizatiti kwenye shinikizo la mbio za kuwania taji la Ligi Kuu England, baada ya kuruhusu uongozi wa mabao mawili kwa moja kuteleza kwenye sare ya 2-2 dhidi ya West Ham Jumapili.

**Arsenal walitangulia kwa mabao 2-0 baada ya dakika 10 tu kwenye Uwanja wa London huku Gabriel Jesus na Martin Odegaard wakifunga.**

Hata hivyo, Arsenal ilishindwa kuendeleza faida hiyo na winga wa West Ham, Said Benrahma alifunga penalti dakika ya 33 na kupunguza bao lao la kuongoza kabla ya Bukayo Saka kukosa mkwaju wa penalti.

Sekunde 140 tu baadaye, West Ham walisawazisha kupitia Jarrod Bowen akielekeza mpira wavuni ndani ya lango la golikipa Aaron Ramsdale na kuwaacha Arsenal kwa pointi nne mbele ya Manchester City, lakini kikubwa zaidi, wakiwa wamecheza mchezo mmoja zaidi na kulazimika kwenda Etihad ndani ya siku 10.

> ●●● Ningesema ndiyo tunashinikiza, lakini lazima tupambane na kujidhatiti...

Alipoulizwa nini matarajio yake kwenye mbio za ubingwa, Arteta aliwaambia waandishi: "Ningesema ndiyo tunashinikiza, lakini lazima tupambane na kujidhatiti.

"Na kwa 2-0, sio shinikizo. Ni kwamba hatukuelewa ni nini mchezo ulihitaji wakati huo. Tulianza vizuri sana, tukatawala mchezo, tukatawala uwanja na kufunga mabao mawili mazuri.

"Baada ya hapo tulifanya makosa makubwa: kuacha kucheza tukiwa na malengo sawa ya kufunga la tatu na la nne na kufikiria tu kwamba tunaweza kucheza karibu nao na kudumisha matokeo.

"Ilionekana kuwa rahisi sana na kwa wakati huo tuliwapa matumaini na sifa kwa West Ham, walichukua. Walienda moja kwa moja - kutoka kwa kurusha kwa muda mrefu hadi kona - na tulijitahidi sana kutoka kwenye mchezo huo.

"Ikiwa hutalinda sanduku lako jinsi unavyopaswa, basi unapaswa kufanya mambo mengi bora kwa muda mrefu zaidi. Kisha kuna wakati unaweza kwenda mbele 3-1 na pengine mchezo umeisha. Lakini hii ni sehemu. Wasiwasi wangu ni baada ya 2-0 tulifanya kosa hilo kubwa na hatukuelewa mchezo ulihitaji nini wakati huo."

"Tulianza kufanya mambo mengi ya kijinga kwenye mpira, tukawaruhusu kucheza kwenye mipira mirefu."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,104,5

JACKPOT
MECHI WIKI HII
TAREHE: 19,20 NA 21 APRILI 2023
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 19/04/23 | 17:00 | Istanbulspor vs Antalyaspor | 2.73 | 3.31 | 2.40 |
| 02. 19/04/23 | 17:00 | Kayserispor vs Kasimpasa | 2.31 | 3.35 | 2.83 |
| 03. 19/04/23 | 18:00 | Fotbal Trinec vs Pribram | 2.68 | 3.09 | 2.42 |
| 04. 19/04/23 | 20:30 | Konyaspor vs Adana Demirspor | 2.61 | 3.30 | 2.51 |
| 05. 19/04/23 | 21:45 | Blackburn vs Coventry | 2.30 | 3.15 | 2.95 |
| 06. 19/04/23 | 21:45 | Swansea vs Preston | 2.44 | 3.16 | 2.76 |
| 07. 19/04/23 | 22:00 | Bayern Munchen vs Manchester City | 2.54 | 3.41 | 2.48 |
| 08. 20/04/23 | 20:30 | Sivasspor vs Trabzonspor | 2.61 | 3.30 | 2.51 |
| 09. 20/04/23 | 22:00 | Sporting Lisbon vs Juventus | 2.34 | 3.17 | 2.97 |
| 10. 21/04/23 | 01:00 | San Lorenzo vs Fortaleza CE | 2.21 | 3.17 | 3.43 |
| 11. 21/04/23 | 05:00 | Universitario vs Goias | 2.23 | 3.12 | 3.01 |
| 12. 21/04/23 | 05:00 | Deportes Tolima vs CA Tigre | 2.27 | 3.28 | 3.17 |
| 13. 21/04/23 | 19:00 | Apollon Limassol vs Pafos FC | 2.44 | 3.27 | 2.74 |

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MAN UNITED WANATAKA MATAJI YOTE - TEN HAG



**MANCHESTER,** England

HUKU kikosi chake cha Manchester United kikiwa bado kinashiriki mbio tatu tofauti za kuwania mataji, kocha Erik ten Hag amesema hatalipa kipaumbele shindano moja kuliko lingine.

"Tupo kwenye michuano tofauti, tunaweza kufanya nini?" Ten Hag alisema baada ya ushindi wa mabao 2-0 wa Ligi Kuu England dhidi ya Nottingham Forest Jumapili.

"Lazima tushinde. Sisi ni United, tunapaswa kushinda kila mchezo."

Ushindi wa United dhidi ya Forest iliyopo kwenye hatari ya kushushwa daraja kwenye Uwanja wa City Ground uliwafanya kushika nafasi ya tatu na kuimarisha uwezekano wa kumaliza katika nafasi nne za juu za Ligi Kuu England.

Mechi hiyo pia ilikuwa kati ya mikondo miwili ya robo fainali ya Ligi ya Europa dhidi ya Sevilla. Baada ya sare ya 2-2 katika mechi ya kwanza, United itaelekea Seville kwa marudiano siku ya Alhamisi.



## Xavi aionya Barcelona isilale

**BARCELONA,** Hispania

XAVI Hernandez ameonya Barcelona wasilale katika mbio za kuwania taji baada ya kulazimishwa sare ya pili mfululizo kwenye Ligi Kuu Hispania, LaLiga, dhidi ya Getafe Jumapili.

Raphinha na Alejandro Balde wote waligonga nguzo katika kipindi cha kwanza huku Barca wakifuatilia matokeo ya juma lililopita dhidi ya Girona wakiwa na pointi nyingi zaidi katika ligi.

Wamesalia na pointi 11 mbele ya Real Madrid kileleni zikiwa zimesalia mechi tisa lakini, huku Atletico Madrid wakiwa katika kiwango bora watakwenda Camp Nou wiki ijayo, na Xavi amesema timu yake inahitaji kurejea kwenye mstari haraka.

"Hatuko katika kiwango chetu bora cha msimu, kulingana na uchezaji au matokeo," alisema baada ya sare ya Getafe.

"Tulijaribu, lakini tulikuwa wavivu sana. Tuna msimu mzuri kwenye LaLiga, lakini hatuwezi kulala sasa. Tuna mechi muhimu zinazokuja."

Baada ya Atletico, Barca watasafiri hadi Rayo Vallecano, ambapo walichapwa msimu uliopita, na kisha kuwakaribisha Real Betis na washindi wa fainali ya Copa del Rey, Osasuna wakijaribu kushinda LaLiga kwa mara ya kwanza tangu mwaka 2019.

## HABARI MICHEZO

80,144/-

# NBC ILIVYONOGESHA ‘DABI’ YA KARIAKOO KWA WATEJA WAKE

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC Bank), ambayo ni mdhamini Mkuu wa Ligi Kuu ya Soka Tanzania Bara, NBC Premiere League, juzi ilinogesha shangwe za mechi ya watani wa jadi Simba na Yanga kwa kuwapeleka uwanjani wateja pamoja na wafanyakazi wake kushuhudia mtanange huo ulioisha kwa timu ya Simba kuibuka na ushindi wa mabao 2-0.

**Zaidi, benki hiyo pia iliandaa ‘Screen’ kubwa kwenye baadhi ya maeneo jijini Dar es Salaam ikiwamo Baa ya Warehouse Arena (zamani Nextdoor Arena) iliyopo Masaki jijini humo ili kutoa fursa kwa wapenzi wa mchezo huo ambao hawakuweza kufika uwanjani.**

Akizungumzia hatua hiyo jana, Mkurugenzi wa Wateja Binafsi wa NBC, Elibariki Masuke, alisema huo ni mwendelezo wa utaratibu wa benki hiyo kutumia mechi hizo maarufu kama ‘Dabi’ ya Kariakoo’ kuandaa matukio yanayolenga kuwakutanisha na wateja wao wakubwa na wadogo ili kufurahia ladha ya ligi hiyo inayoendelea kujiongezea umaarufu barani Afrika kufuatia udhamini mnono walioufanya.

“Umekuwa ni utaratibu wetu sasa kufurahia na wateja wetu kwa namna mbalimbali inapofika siku kama ya leo [juzi] ambapo miamba miwili ya soka letu inapokutana uwanjani. Kwa kutambua ile pressure wanayokuwa nayo wateja wetu kwenye mechi hizi tumekuwa tukiwaandalia matukio kadhaa ili tu tuwe nao karibu siku hiyo kubwa.” alisema.

Aidha, juzi kama ilivyokuwa kwenye dabi iliyopita, ilishuhudiwa wateja hao wakipata chakula cha mchana kwenye Hoteli ya Hyatt The Kilimanjaro iliyopo jijini Dar es Salaam sambamba na viongozi wa benki hiyo tukio lilitofuatiwa na msafara maalum wa ‘marafiki’ hao kuelekea Uwanja wa Benjamin Mkapa kushuhudia mtanange huo kwa udhamini wa benki hiyo kabla ya kurejeshwa salama baada ya kumalizika kwa mechi hiyo.

“Kwa wale ambao wanakosa nafasi hii ya kufika uwanjani pia tunawaandalia mazingira mazuri kwa kuwawekea screen kubwa kwenye baadhi ya maeneo ikiwamo baa maarufu zilizopo karibu na maeneo yao,” alisema Masuke.

Mbali na kutoa fursa kwa wapenzi wa soka kufuatilia mechi hiyo kupitia screen kubwa pia wateja hao walipata fursa ya kupata huduma mbalimbali za kifedha kutoka NBC kupitia maofisa wa benki hiyo waliokuwa wakitoa huduma mbalimbali ikiwamo kufungua akaunti mbalimbali pamoja na kufanya miamala ya kifedha wakiwa maeneo hayo na viunga vya Uwanja wa Benjamin Mkapa.



Mkurugenzi wa Wateja Binafsi wa Benki ya NBC, Elibariki Masuke (Kulia), akizungumza na baadhi wa wateja wa benki hiyo wakati wa hafla ya chakula cha mchana muda mfupi kabla ya wateja hao kuelekea Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kushuhudia mechi ya ‘dabi’ kati ya Simba na Yanga iliyopigwa mwishoni mwa wiki ikiwa ni muendelezo wa utaratibu wa benki hiyo kutoa fursa kwa wateja wake ambao ni wapenzi wa mchezo huo kuweza kufurahia mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara wanayoidhamini. **MPIGAPICHA WETU**

## Mtanzania Geay

INATOKA UK. 24

kwa umbali wa kilometa 11 hadi 20, lakini alionekana ‘kukata moto’ robo ya mwisho kutokana na kupambana na wanariadha wengi vijana.

Nafasi ya nne ilichukuliwa pia na Mkenya Albert Kirir aliyemaliza kwa saa 2:08:01, huku raia wa Morocco Zouhair Talbi akimaliza wa tano kwa kutumia saa 2:08:35.

Kwa upande wa wanawake, Wakenya pia walitawala mbio hizo za Boston Marathon, pale Hellen Obiri alipoibika mshindi wa kwanza, akibimbia kwa saa 2:21:28, akifuatiwa na Amane Beriso kutoka Ethiopia aliyemaliza kwa saa 2:21:50, huku Lonah Salpeter raia wa Israel akishika nafasi ya tatu kwa kutumia muda wa saa 2:21:57.

## Robertinho atoa siri

INATOKA UKURASA 24

akaunti ya Rais Samia kwa niaba ya klabu yake.

Akaunti rasmi ya klabu ya Simba nayo iliandika kwa kushukuru na kupokea pongezi hizo, ikiahidi kuwa timu yao itafanya vema tena kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

“Asante sana Mheshimiwa Samia, tunakuahidi ushindi mkubwa zaidi kwenye michezo iliyo mbele yetu ukiwamo wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Wydad Athletic Club,” iliandika akaunti hiyo ya Instagram.

Akizungumza baada ya mechi hiyo, Afisa Mtendaji Mkuu, Kajula alisema mechi hiyo dhidi ya watani zao wa jadi kilikuwa ni kipimo kizuri kabla ya mchezo wa Jumamosi dhidi ya Wydad.

“Nafurahi kwa sababu huu ni mwendelezo mzuri kujiandaa na mechi ya Wydad siku ya Jumamosi. Tuna ari nzuri, na hata kukosekana kwa wachezaji wetu wengi kama Sadio Kanoute ambaye ni majeruhi, lakini kwenye mechi itakayokuja atakuwapo na Aishi Manula,” alisema Kajula.



## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 22/04.23 | 17:00 | Brentford FC vs Aston Villa | 2.41 | 3.20 | 2.75 |
| 02. 22/04.23 | 17:00 | Leicester City vs Wolverhampton Wanderers | 2.38 | 3.15 | 2.85 |
| 03. 22/04.23 | 19:30 | Preston North End vs Blackburn Rovers | 2.46 | 3.20 | 2.70 |
| 04. 22/04.23 | 21:00 | FC Groningen vs NEC Nijmegen | 2.75 | 3.15 | 2.44 |
| 05. 22/04.23 | 21:45 | Sampdoria Genoa vs Spezia Calcio | 2.46 | 3.10 | 2.75 |
| 06. 23/04.23 | 10:00 | Kawasaki Frontale vs Urawa Red Diamonds | 2.37 | 3.10 | 2.55 |
| 07. 23/04.23 | 13:30 | Kasimpasa Istanbul vs Konyaspor | 2.47 | 3.25 | 2.35 |
| 08. 23/04.23 | 15:30 | PSV Eindhoven vs Ajax Amsterdam | 2.32 | 3.40 | 2.75 |
| 09. 23/04.23 | 16:00 | AFC Bournemouth vs West Ham United | 2.85 | 3.15 | 2.39 |
| 10. 23/04.23 | 16:00 | AC Ajaccio vs Stade Brest 29 | 2.95 | 3.00 | 2.42 |
| 11. 23/04.23 | 18:05 | Montpellier HSC vs Stade Rennes | 2.95 | 3.30 | 2.24 |
| 12. 23/04.23 | 18:30 | Brighton & Hove Albion vs Manchester United | 2.32 | 3.45 | 2.70 |
| 13. 23/04.23 | 18:30 | Bayer Leverkusen vs RB Leipzig | 2.55 | 3.40 | 2.49 |
| 14. 23/04.23 | 20:30 | Borussia Monchengladbach vs Union Berlin | 2.28 | 3.20 | 2.95 |
| 15. 23/04.23 | 21:45 | Juventus Turin vs SSC Napoli | 2.75 | 3.05 | 2.50 |
| 16. 23/04.23 | 21:45 | Olympique Lyon vs Olympique Marseille | 2.37 | 3.45 | 2.65 |
| 17. 23/04.23 | 22:00 | Sevilla FC vs Villarreal CF | 2.85 | 3.25 | 2.34 |

## MECHI ZA USHINDI

“1” NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA “X” NI TIMU KUTOKA SARE “2” NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JAMANNE - 18/04/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 3418 | Bucheon vs Seoul E Land | 2.30 | 2.98 | 2.93 |
| 13:00 | 5430 | Cheongju FC vs Chungnam Asan | 2.24 | 3.04 | 2.99 |
| 13:30 | 5275 | Gyeongnam vs Anyang | 2.62 | 2.97 | 2.55 |
| 19:30 | 3341 | Admira Wacker vs Kapfenberg | 1.64 | 3.84 | 4.36 |
| 19:30 | 3696 | Vorwarts Steyr vs Amstetten | 2.69 | 3.32 | 2.34 |
| 20:00 | 2487 | GIF Sundsvall vs Ostersunds | 2.20 | 3.30 | 3.19 |
| 20:30 | 2775 | Fatih Karagumruk vs Umraniyespor | 1.82 | 3.79 | 3.68 |
| 20:30 | 3484 | Marumo Gallants FC vs SuperSport Utd | 3.25 | 2.78 | 2.37 |
| 20:30 | 4413 | Alanyaspor vs Galatasaray | 4.84 | 4.10 | 1.58 |
| 21:00 | 3945 | AL Bataeh (UAE) vs Dibba Al Fujairah | 2.09 | 3.45 | 2.93 |
| 21:00 | 4864 | Al Dhafra vs AL Khaleej Khor Fakkan | 3.14 | 3.39 | 2.01 |
| 21:00 | 4872 | Al Nasr Dubai vs Shabab AL Ahli Dubai Club | 4.61 | 3.79 | 1.59 |
| 21:00 | 5660 | AL Wahda Scc (UAE) vs Jazira Abu Dhabi | 2.16 | 3.33 | 2.87 |
| 21:45 | 1198 | Oxford Utd vs Portsmouth | 2.24 | 3.29 | 3.04 |
| 21:45 | 1372 | Stoke City vs Wigan | 1.54 | 3.84 | 5.59 |
| 21:45 | 1487 | Falkirk FC vs Edinburgh City | 1.61 | 3.86 | 4.69 |
| 21:45 | 1605 | Rotherham vs Burnley | 5.01 | 3.65 | 1.62 |
| 21:45 | 1849 | Sunderland vs Huddersfield | 1.64 | 3.75 | 4.70 |
| 21:45 | 1917 | Lincoln vs Barnsley | 3.84 | 3.34 | 1.92 |
| 21:45 | 2030 | Salford City vs Hartlepool | 1.50 | 4.05 | 5.34 |
| 21:45 | 2239 | Dumbarton vs Stirling | 2.98 | 3.70 | 1.98 |
| 21:45 | 2660 | Ipswich vs Port Vale | 1.24 | 5.45 | 11.09 |
| 21:45 | 2866 | Carlisle vs Stockport | 2.74 | 2.99 | 2.49 |
| 21:45 | 2964 | Gillingham vs Leyton Orient | 2.87 | 3.02 | 2.38 |
| 21:45 | 3171 | Sutton United vs Northampton | 2.28 | 3.12 | 2.93 |
| 21:45 | 3203 | Rochdale vs Tranmere | 2.37 | 3.08 | 2.83 |
| 21:45 | 3336 | Harrogate vs Walsall | 2.43 | 3.11 | 2.72 |
| 21:45 | 3470 | Wrexham vs Yeovil | 1.15 | 6.71 | 14.67 |
| 21:45 | 3623 | Halifax vs Bromley | 2.50 | 3.27 | 2.64 |
| 21:45 | 3704 | Bristol Rovers vs Sheffield Wed | 4.44 | 3.68 | 1.71 |
| 21:45 | 3741 | Stevenage vs Doncaster | 1.39 | 4.26 | 6.93 |
| 21:45 | 3764 | Hamilton vs Inverness | 2.96 | 3.27 | 2.22 |
| 21:45 | 4004 | Blackpool vs West Bromwich | 3.51 | 3.36 | 1.97 |
| 21:45 | 4101 | Sheffield Utd vs Bristol City | 1.50 | 4.00 | 5.80 |
| 21:45 | 4209 | Shrewsbury vs Plymouth | 3.53 | 3.43 | 1.98 |
| 21:45 | 4492 | Exeter vs Derby | 3.28 | 3.33 | 2.11 |
| 21:45 | 4730 | Forest Green vs Fleetwood Town | 3.12 | 3.17 | 2.25 |
| 21:45 | 4937 | Grimsby vs Barrow | 2.16 | 3.17 | 3.12 |
| 21:45 | 5061 | Burton vs Bolton | 3.23 | 3.43 | 2.09 |
| 21:45 | 5261 | Newport vs Mansfield | 2.58 | 3.08 | 2.58 |
| 21:45 | 5316 | Crawley Town vs Colchester | 2.82 | 3.11 | 2.36 |
| 21:45 | 5526 | Cambridge Utd vs Wycombe | 2.58 | 3.29 | 2.58 |
| 21:45 | 5570 | MK Dons vs Charlton | 2.40 | 3.23 | 2.83 |
| 21:45 | 5778 | Accrington vs Peterborough | 4.13 | 3.73 | 1.75 |
| 21:45 | 5803 | Swindon Town vs Bradford City | 3.07 | 3.27 | 2.13 |
| 22:00 | 4040 | Al Hilal Riyadh vs Al Nasr Riyadh | 2.06 | 3.47 | 3.37 |
| 22:00 | 4160 | Napoli vs AC Milan | 1.78 | 3.36 | 4.32 |
| 22:00 | 4214 | Chelsea vs Real Madrid | 2.64 | 3.28 | 2.46 |
| 22:00 | 5309 | Millwall vs Birmingham | 1.74 | 3.36 | 4.62 |
| 22:15 | 1129 | Pyramids vs El Daklyeh | 1.43 | 4.23 | 6.65 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.



Arteta: Arsenal ina kazi kubwa UKURASA 21

MGUU KWA MGUU...




Mwanariadha wa Tanzania, Gabriel Geay (kulia), akichuana vikali na Evans Chebet wa Kenya, kwenye mbio za Boston Marathon zilizofanyika jana nchini Marekani, kabla ya Mkenya huyo kushinda akitumia muda wa saa 2:05:54 dhidi ya 2:06:04 wa Geay aliyeshika nafasi ya pili. **PICHA: MTANDAO**

## Mtanzania Geay ashika nafasi ya pili Boston Marathon

**BOSTON,** Marekani

MWANARIADHA wa Kenya, Evans Chebet, ameshinda kwa mara ya pili mfululizo mbio za Boston Marathon akitumia muda wa saa 2:05:54 huku akifuatiwa na Mtanzania Gabriel Geay aliyetumia muda wa saa 2:06:04.

Huo ni ushindi wa tatu mkubwa kwa Chebet katika wasifu wake, huku anayeshikilia rekodi ya dunia ya marathon, Eliud Kipchoge akishindwa kuonyesha uhodari wake katika mbio hizo.

Chebet, ambaye ni mshindi wa mwaka 2021 ametwaa tena medali hiyo huku Benson Kipruto na Gabriel Geay wakimpoteza kwa mbali Kipchoge.

Geay alishinda mbio hizo kwa mara ya pili, akiachwa sekunde 10 nyuma na sekunde mbili mbele ya Kipruto huku Kipchoge, mshindi wa mashindano makubwa ya marathon mara 12, akishika nafasi ya sita baada ya kutumia muda wa saa 2:09:23.

Mtanzania huyo alifanya kazi ya ziada kukabiliana na wanariadha wa Kenya waliomuweka 'mtu kati', lakini alifanikiwa kupambana hasa kwenye hatua za mwisho za mbio hizo, akimchomoka Kipruto wa Kenya aliyekuwa naye sambamba, kabla ya kumaliza mbio hizo akitumia saa 2:06:04.

Geay alijitahidi kupambana na wanaridha saba alioonekana kwenda nao sambamba katikati ya mbio hizo na kuna wakati aliongoza kwa dakika kadhaa kabla ya Chebet na Kipruto kumkuta. Kipchoge, 38 ambaye aliwaongoza wenzake

INAENDELEA UKURASA 23

# ROBERTINHO ATOA SIRI YA KUIKANDA YANGA

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

## Rais Samia aipongeza, waahidi kumfurahisha zaidi Jumamosi dhidi ya Wydad Casablanca, huku...

HUKU Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan kupitia ukurasa wake wa mtandao wa kijamii akipongeza Simba kwa ushindi walioupata dhidi ya Yanga kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara juzi, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mbrazili Robertinho Oliveira, ametoa siri ya ushindi huo.

**Katika mchezo huo uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Simba iliibuka na ushindi wa mabao 2-0, shukrani kwa Henock Inonga aliyeanza kutupia dakika ya pili kwa kichwa kabla ya 'fataki' kali la Denis Kibu dakika ya 31 ya mchezo.**

Akizungumzia mchezo huo, Kocha Mkuu wa Simba, Robertinho, alisema siri ya ushindi dhidi ya Yanga, mbali na mbinu alizowapa wachezaji, lakini pia ni mahusiano mazuri aliyotengeneza kati yake na wachezaji.

Alisema katika mchezo huo, lengo lao lilikuwa kutafuta bao la mapema na walifanikiwa kwa kupata bao dakika ya pili na baada ya hapo waliongeza kasi ya kutafuta jingine hali iliyowafanya wapinzani wao Yanga kutoka mchezoni.

Kocha huyo alisema baada ya kupata bao la kwanza walipoteza nafasi nyingine mbili za haraka kupitia kwa Jean Baleke na hali hiyo ilizidi kuwachanganya wapinzani wao jambo ambalo lilichangia kupata matokeo chanya katika 'dabi' hiyo.

"Nilisema jana (Ijumaa), nazipenda sana mechi za dabi na leo (juzi) nimeshinda kama ambavyo nimewahi kushinda dabi za huko nyuma, nimpongeze pia Ally ( Salim) kwa mchezo mzuri leo na nimeamua kumuamini kwa sababu ndiye aliyekuwapo na alifanya vizuri mchezo uliopita.

"Kumbuka tulikuwa ugenini bila Aishi pamoja na mlinda mlango namba mbili Beno [Kakolanya], alicheza vizuri na leo [juzi] pia tukaamua kumuamini," alisema na kuongeza:

"Kila mchezaji ndani ya Simba ana mchango na kilichonifurahisha kila mtu alicheza kwa kujituma na kucheza kwa ushirikiano wa juu, zaidi nawapongeza wachezaji wangu wote."

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, alipongeza Simba kwa ushindi walioupata, lakini akasema hakufurahishwa na maamuzi ya mwamuzi Jonesiya Rukyaa.

Alisema wachezaji hawakucheza vizuri kipindi cha kwanza kitu kilichotoa nafasi kwa wapinzani wao kutawala eneo la kiungo, lakini kipindi cha pili walijipanga vizuri na kutengeneza nafasi nyingi, ila walishindwa kuzitumia.

"Tunakubali matokeo, lakini sikufuraishwa na maamuzi ya mwamuzi, aliisaidia sana Simba mfano mpira wa kona uliozaa bao la kwanza, pia kulikuwa na filimbi nyingi za faulo ambazo zote zilikuwa zinaelekezwa kwetu na kuwatoa wachezaji wangu mchezoni baada ya kufungwa bao la mapema.

"Hatukatai kufungwa, lakini tunataka iwe halali siyo tunachezeshwa na mwamuzi ambaye hana hofu ya Mungu, naomba usiniulize kuhusu Robertinho sijui Mourinho, ulinza kuhusu Simba na Yanga, siku nyingine tunataka waamuzi wenye hofu ya Mungu," alisema kocha huyo raia wa Tunisia.

Baada ya ushindi huo, Rais Samia kupitia ukurasa wake wa Instagramu, aliipongeza Simba kwa kuandika: "Hongereni Simba kwa ushindi wenu dhidi ya Yanga katika mchezo wa Ligi Kuu ya Tanzania Bara. Upinzani wenu wa jadi uwanjani ni burudani inayowaleta pamoja mamilioni ya Watanzania katika kila kona ya nchi yetu, kwa namna ya kipekee."

Pongezi hizo zilipokelewa na Wanasimba na kumuahidi ushindi mkubwa zaidi kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika Jumamosi ijayo dhidi ya Mabingwa wa Afrika, Wydad Casablanca ya Morocco, huku pia wakiahidi kudumisha na kutunza amani, upendo na umoja.

"Ahsante sana Mheshimiwa Rais, tunashukuru kwa sapoti yako kubwa kwenye sekta ya michezo, tutaendelea kutumia mpira wa miguu kuunganisha Watanzania pia kutunza amani, upendo na umoja. Leo (juzi) tumekupa mkono wa Eid mapema," Afisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Imani Kajula, aliandika akipokea na kushukuru pongezi hizo kwenye

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >